# Nipashe

Jumatatu Aprili 3, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581269

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US





UKURASA 11


MID WEEK JACKPOT!

TZS. 536,262,050

KWA TZS. 1000 TU!

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SportPesa.CO.TZ

PIGA *150*87#




## Mfanyabiashara mbaroni kukutwa na chakula cha ruzuku

UKURASA 5

# Kichaka kipya ufisadi nchini

• **Bil**. 190/- zaliwa na 'watu hewa', Samia ashtuka... *Ukurasa 2*



Rais Samia Suluhu Hassan akimuapisha George Simbachawene kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora), Ikulu jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

## DC: Marufuku kuuza mahindi yakiwa shambani

UKURASA 4

UKURASA WA 4

### TFS YAHOFU ONGEZEKO MIFUGO KUINGIA MISITU HIFADHI

MHIFADHI Mkuu wa Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), Wilaya ya Rufiji mkoani Pwani, Francis Kiondo, amesema kumekuwa na ongezeko kubwa...

UKURASA WA 7

### RITA KUTOA HUDUMA ZOTE KIDIJITALI

WAKALA wa Usajili Ufilisi na Udhamini (RITA), umetambulisha mfumo mpya wa kutoa huduma zake zote kidijitali unaofahamika kama e-RITA.

# PM azigeukia taasisi za dini wanaokiuka maadili

UKURASA 3



Waamini wa Kanisa la Anglikana Kristo Mfalme, Kinondoni, Dar es Salaam wakiwa katika ibada ya Sikukuu ya Matawi, jana. Picha ndogo: Padri Kiongozi wa Kanisa hilo, Jerome Napela akiongoza ibada hiyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**


**MICHEZO** ROBERTINHO HESABU DARAJA YANGA CAF UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

# Kichaka kipya ufisadi nchini

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

SASA ni dhahiri mikopo ya halmashauri kwa makundi maalum imekuwa kichaka kipya cha ufisadi wa mabilioni nchini.

Kwanini? Katika miaka sita ya fedha iliyopita (2016/17-2021/22), jumla ya Sh. bilioni 192 hazijarejeshwa na wanufaika wa mikopo hiyo huku Rais Samia Suluhu Hassan akikiri kuwa fedha hizo hazikusanyiki tena kutokana na vikwazo mbalimbali ikiwamo kukopeshwa kwa 'watu hewa'.

Katika ripoti yake ya ukaguzi kwa mwaka 2020/21 iliyowasilishwa bungeni Aprili 12, mwaka jana, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), alibaini mabilioni ya shilingi yako hatarini kupotea kutokana na kutokuwa na udhibiti mzuri wa usimamizi wa mikopo inayotolewa na halmashauri kwa makundi maalum.

CAG Charles Kichere alibainisha kuwa kwa mwaka huo wa ukaguzi, halmashauri 155 hazikukusanya Sh. bilioni 47.01 za marejesho ya mikopo iliyotolewa kwa makundi hayo.

Kwa mujibu wa CAG, hali iliyobainika katika ukaguzi wake wa mwaka 2020/21 ni mwendelezo wa kile alichokibaini katika miaka mitano iliyopita kuhusu mikopo hiyo.

| Mwaka | Hal. | Kisichorejeshwa | Asilimia |
|---|---|---|---|
| 2020/21 | 155 | Bil 47/- | 70 |
| 2019/20 | 130 | Bil 27.79/- | 65 |
| 2018/19 | 111 | Bil. 13.79/- | 59 |
| 2017/18 | 90 | Bil 10.04/- | 59 |
| 2016/17 | 84 | Bil 5.81/- | 63 |

**Jedwali la mikopo isiyorejeshwa inayotolewa na serikali kwa makundi maalum kupitia asilimia 10 ya mapato ya halmashauri nchini. CHANZO: RIPOTI YA CAG 2020/21.**

Katika mukhtasari wa ripoti yake ya ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2021/22 aliyoiwasilisha kwa Rais Samia Jumatano ya wiki iliyopita, CAG Kichere alibainisha kuwa Sh. bilioni 88 zilizokopeshwa na halmashauri kwa makundi maalum kwa mwaka huo wa fedha, hazijakusanywa.

Hii ina maana kwamba kuanzia mwaka wa fedha 2016/17 hadi mwaka uliopita wa fedha, jumla ya Sh. bilioni 192 hazijakusanywa kutoka kwa wanufaika wa mikopo hiyo.

**UCHUNGUZI WA CAG**

Katika ripoti yake ya 2020/21, anabainisha kuwa katika kufuatilia uzingatiaji wa matakwa ya sheria iliyopo, alibaini wanufaika wa vikundi katika mamlaka 155 za serikali za mitaa hawakurejesha Sh. bilioni 47.01 kama marejesho ya mkopo waliopewa.

CAG pia anasema alibaini mamlaka 83 za serikali za mitaa hazikuchangia Sh. bilioni 6.68 katika mfuko kama inavyotakiwa kisheria, jambo ambalo linazuia azma ya serikali ya kuwawezesha kiuchumi wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kwa lengo la kupunguza umaskini.

"Pia nilibaini mikopo yenye thamani ya Sh. milioni 178.61 ilitolewa kwa vikundi visivyokuwa na sifa na Sh. bilioni 1.24 hazikuhamishwa kutoka akaunti za amana za mamlaka 11 za serikali za mitaa (halmashauri) kwenda akaunti maalum ya mfuko, kinyume cha Kanuni ya 22(1) na (2) ya Mfuko wa Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu," CAG anabainisha.

Anazitaja halmashauri ambazo hazikuhamishia Sh. bilioni 1.24 katika akaunti maalum za mikopo ni: Ushetu (Sh. 308,528,550); Bahi (Sh. 54,222,488); Iringa (Sh. 236,486,588); Busega (Sh. 49,090,000); Nanyumbu (Sh. 179,268,173); Momba (Sh. 41,795,000); Kilolo (Sh. 122,596,622); Gairo (Sh. 38,679,672); Rungwe (Sh. 115,777,111); Ileje (Sh. 32,043,700); na Sengerema (Sh. 59,511,900).

**SHIDA ILIPO**

CAG anabainisha kuwa kutorejeshwa kwa mikopo hiyo kunatokana na kutokuwa na udhibiti mzuri wa usimamizi wa mikopo, akifafanua kuwa mamlaka za serikali za mitaa husika zilitoa mikopo kabla ya kufanya uchambuzi wa kina wa historia ya ulipaji wa kikundi na kupitia mapendekezo ya mradi husika ili kuhakikisha kikundi kina uwezo wa kurejesha mkopo kwa wakati.



CAG Charles Kichere

Vilevile, CAG anasema amebaini hakuna ufuatiliaji wa karibu wa kukusanya marejesho ya mikopo ambayo bado haijalipwa kutoka kwenye vikundi.

Ili kufikia lengo na uendelevu wa mfuko, CAG anasisitiza mamlaka za serikali za mitaa kufanya tathmini kabla ya kutoa mikopo na kuweka juhudi zaidi katika kukusanya madeni ambayo hayajalipwa.

Pia anaishauri Ofisi ya Rais - TAMISEMI ianzishe hatua madhubuti za kurejesha mikopo kwa kuhusisha wataalamu wa usimamizi wa mikopo ambao watahimiza uzingatiaji wa urejeshaji wa mikopo kwa hiari ili kufikia ukuaji endelevu wa mfuko.

CAG pia anabainisha kuwa tathmini aliyoifanya katika akaunti za benki za biashara ambako mamlaka za serikali za mitaa hutunza fedha za mfuko, ilibainisha Sh. milioni 156.23 za mfuko zililimbikizwa katika akaunti kwa zaidi ya mwaka mmoja bila kukopeshwa kwa wanufaika pasipokuwa na sababu za msingi.

Halmashauri zilizokuwa na bakaa ya muda mrefu katika benki za biashara ni za wilaya za Mpwapwa (Sh. 108,703,450) na Nyasa (Sh. 47,530,700).

Anataja dosari nyingine katika mikopo hiyo ni kutoshirikishwa kwa wataalamu wa usimamizi wa mikopo katika mchakato wa utoaji na urejeshwaji wa mikopo.

"Nilibaini kuwa uhakiki wa vikundi vilivyoomba mikopo ulikuwa haufanyiki kabisa kabla ya mikopo kutolewa. Hii ni kutokana na ukosefu wa utaalamu wa kufanya uhakiki unaostahili katika mikopo.

Anasisitiza mamlaka za serikali za mitaa kufanya tathmini kabla ya kutoa mikopo na kuweka juhudi zaidi katika kukusanya madeni ambayo bado hayajalipwa.

Aidha, TAMISEMI ianzishe hatua madhubuti za kurejesha mikopo kwa kuhusisha wataalamu wa usimamizi wa mikopo ambao watahimiza uzingatiaji wa urejeshaji wa mikopo kwa hiari ili kufikia ukuaji endelevu wa mfuko.

"Ninapendekeza kuwa Ofisi ya Rais - TAMISEMI itumie benki za serikali au wataalamu wa usimamizi wa dhamana na uwekezaji kama vile Benki ya Maendeleo na Benki ya Biashara Tanzania katika kuongeza ufanisi kwenye kutoa, kufuatilia na kusimamia urejeshwaji wa mikopo na kwa kuzingatia gharama nafuu ya uendeshaji.

**USULI NA HISTORIA**

Inaporejewa historia ya mikopo hiyo, inaonyesha kwamba, mwaka 1993 serikali kupitia Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ilianzisha Mfuko wa Fedha wa Maendeleo kwa Wanawake na Vijana ili kuwainua kiuchumi ambao wengi wao hawakidhi vigezo vya mikopo inayotolewa na taasisi za fedha kutokana na ukosefu wa dhamana.

Kwa wakati huo, mikopo hiyo ya uwezeshaji ilitolewa asilimia tano kwa wanawake na asilimia tano kwa vijana.

Mwaka 2019, serikali kupitia Bunge, ilirekebisha Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura ya 290 (iliyorejewa 2019) kwa kuongeza kifungu cha 37A mahususi kwa ajili ya kuwezesha mikopo kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

Vilevile, Kanuni za Utoaji na Usimamizi wa Mikopo kwa Vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu, 2019 (Tangazo la Serikali Na. 286 la 5/04/2019) zinataka mamlaka zote za serikali za mitaa kutenga asilimia 10 ya mapato yatokanayo na vyanzo vya ndani ili kutoa mikopo isiyo na riba kwa vikundi vilivyosajiliwa vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

Madhumuni ya mfuko huo ni kuongeza uwezeshaji kiuchumi kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kwa kufanya shughuli za kiuchumi ili kuboresha kiwango chao cha maisha.

**SAMIA ASHTUKA**

Baada ya kupokea ripoti mpya ya CAG Jumatano ikionyesha kwa mwaka 2021/22 Sh. bilioni 88 zilizotolewa na halmashauri kama mikopo kwa vikundi vya wanawake, vijana na wenye ulemavu hazikurejeshwa, alisema kadhia hiyo inasababishwa na utaratibu mbovu wa utoaji mikopo hiyo na ufuatiliaji hafifu.

Marekebisho yanayotajwa na Rais Samia yanahusu kubadili mfumo wa utoaji mikopo hiyo kutoka halmashauri ili kazi hiyo ifanywe na benki ambayo itakuwa imeteuliwa na serikali kusimamia jambo hilo, ushauri ambao ulitolewa na CAG katika ripoti ya mwaka 2020/21.

**WACHAMBUZI WASHAURI**

Mwanasiasa Dk. Godbertha Kinyondo, alisema tatizo hilo linatokana na watumishi kutokuwa na elimu ya kutosha kuhusu masuala ya mikopo na fedha hali inayosababisha kutokuwa makini wakati wanatoa mikopo na ufuatiliaji wake.

Kufuatia hali hiyo ameishauri serikali ishirikiane na sekta binafsi zenye ujuzi wa fedha ili wafanye kazi ya kutoa mikopo kwa makubaliano maalum, kwamba hiyo itasaidia kuondoa hasara ya kupotea pesa na suala la kutoa mikopo kwa kujuana.

Ofisa Mkuu Mtendaji wa Taasisi ya Uongozi na Maendeleo ya Ujasiriamali (IMED), Dk. Donath Olomi, alisema serikali itafute namna ya kuwabana wanasiasa wasizitumie pesa hizo kwa maslahi yao binafsi kwa sababu baadhi yao hasa madiwani wamekuwa wakishawishi pesa hizo zitolewe kwa baadhi ya vikundi kwa nia ya kuwavutia wawapigie kura.

"Yule anayepewa zile pesa anaona hakuna umuhimu wa kuzirudisha kwa sababu aliyempa ameshamwambia sababu ni ampigie kura na yeye kura keshampigia anahesabu kama ameshamlipa, sasa nguvu ya kumdai mtu kama huyo inatoka wapi? alisema Dk. Olomi.



Dk. Donath Olomi

**HABARI KITAIFA**

# Majaliwa awageukia viongozi ukiukwaji wa maadili

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amewataka viongozi wa dini wanapopata nafasi kwenye mimbari wakemee kuhusu ukatili wa kijinsia pamoja na wanaoenda kinyume na maadili na desturi za kitanzania.

Alitoa rai hiyo jana jijini Dar es Salaam wakati akizungumza na viongozi na waumini waliohudhuria mashindano ya kitaifa ya kuhifadhi Quran tukufu.

Mashindano hayo yaliandaliwa na Taasisi ya Aisha Sururu Foundation (ASF).

"Nitoe rai kwa viongozi wetu wa dini muendelee kutoa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa kulinda mila, desturi na tamaduni za kitanzania hususani katika kipindi hiki tunachokabiliwa na wimbi kubwa la mmomonyoko wa maadili," alisema Majaliwa na kuongeza:

"Sasa hivi Tanzania inakabiliwa na tatizo la mmomonyoko wa maadili na pia kumeibuka wimbi la vitendo vingine ambavyo vinakwenda kinyume kabisa na dini zetu pamoja na mila, desturi na tamaduni za kitanzania.

Ninampongeza sana Dk. Aboubakar bin Zubeir, Mufti na Shekhe Mkuu wa Tanzania kwa kulisimamia kidete suala hili ikiwa ni pamoja na kutoa maelekezo mahsusi kwa viongozi wote wa Baraza Kuu la Waislamu Tanzania kulikemea na kutolifumbia macho."

Alisema licha ya kukithiri kwa vitendo hivyo, Waislamu wanajivunia uwapo wa Quran tukufu ambayo katika sura ya 33 aya ya 21 (Quran 33:21) wanakumbushwa kwamba wanacho kiigizo chema kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu.

Waziri Mkuu alisema: "Tunapowahifadhisha Quran vijana wetu, tuhakikishe jambo hilo jema linakwenda sambamba na ujenzi wa misingi imara ya malezi itakayowafanya wawe raia wema, waadilifu na wazalendo kwa nchi yao. Tukiwa wazazi, walezi na walimu wa Quran, nitoe rai kwamba tunapotoka hapa hebu tujiulize ni kwa kiasi gani tunaizingatia hii Quran tukufu katika mwenendo mzima wa maisha yetu ya kila siku."

Alisema kwa kufanya hivyo watakuwa wanamsaidia Rais Samia Suluhu Hassan ambaye mara zote amekuwa akiguswa na suala zima la maadili hususan kwa vijana.

Waziri Mkuu aliwaomba waumini hao waendelee kuiombea amani Tanzania kwa kuwa ikipotea mikusanyiko kama hiyo haitofanyika.

Alisema Quran sura ya pili aya ya 126 (Quran 2:126) inawakumbusha umuhimu wa kuiombea nchi amani kupitia dua ya Nabii Ibrahimu alipouombea mji wake na wakazi wake amani na neema.

Shekhe Mkuu na Mufti wa Tanzania, Dk. Aboubakar bin Zubeir, alimpongeza Mwenyekiti wa Taasisi ya ASF, Aisha Sururu kwa kuandaa mashindano hayo kwa miaka 22 na kumueleza kwamba ni mwanamke pekee Tanzania na Afrika Mashariki ambaye anafanya kazi hiyo.

# Ulega: Tunaboresha sera ya mifugo ilete mchango

**Na Jenifer Gilla**

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, amesema wizara ipo katika hatua ya mwisho ya kuboresha sera ya mifugo ya mwaka 2006, ili ilete mchango chanya katika maendeleo ya nchi.

Aliyasema hayo juzi kupitia mtandao wa 'Club house' wakati akichangia mada ya mwelekeo na mageuzi katika sekta hiyo na kuongeza kuwa wizara imejipanga kuhakikisha kuwa mifugo na uvuvi vinateka soko la kimataifa.

Ulega alisema maboresho hayo ni moja ya mikakati ya wizara hiyo ya kuleta mageuzi katika sekta za mifugo na uvuvi na kwa sasa wataalam wanamalizia kuipitia ili ipelekwe katika mchakato wa kisheria kwa ajili ya kupitishwa na kuanza kazi.Alisema mkakati mwingine ni kuhamasisha na kufuatilia utoaji wa chanjo kwa kufuata utaratibu maalum kwa mujibu wa Sheria ya Ugonjwa wa Mifugo namba 17 ya Mwaka 2003 ili kuboresha na kutunza mifugo hiyo na kufikia viwango vya kuuza kimataifa.

Aidha, wana mpango wa kuboresha upatikanaji wa majani na maji ili kuhakikisha mifugo haifariki kwa kukosa malisho na kuondoa migogoro inayoendelea kati ya wakulima na wafugaji kutokana na mifugo kuvamia mashamba kunakosababishwa na uhaba wa chakula.

Kuhusu uvuvi, Ulega alisema mwaka wa fedha 2022/2023 serikali ilitoa Sh. bilioni 20 kati ya hizo Sh. bilioni 17.5 zilitolewa kwa ajili ya kuboresha ufugaji wa samaki kwa njia ya vizimba katika Ziwa Victoria, lengo likiwa ni kukuza ubora wa bidhaa hiyo ili ikubalike sokoni.

Alisema lengo la wizara ni kukuza soko la mifugo ndani na nje ya nchi ikiwamo kuuza nyama nje ya nchi, huku Watanzania wakila nyama za kutosha ili kuwaepusha na magonjwa yanayosababishwa na ukosefu wa protini ikiwamo udumavu.

"Tumeshafika hatua ya kuuza tani 12,000 mpaka 14,000 ambapo tumetoka katika kuuza tani 1,700, lakini tunaona kuna nafasi ya kuuza zaidi duniani katika masoko mbalimbali," alisema Ulega.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA WILAYA YA NYAMAGANA**
**SHAURI LA MIRATHI NO.26/2023**

**YEKUNO S/O AMLAK CHITEJI ..........MSIMAMIZI**
**DHIDI YA**
**FRANK MATHEW CHITEJI...............MAREHEMU**

**KWA: YEYOTE ANAYEHUSIKA**
**KUITWA SHAURINI**

Mwombaji mtajwa hapo juu amefungua shauri la mirathi katika mahakama hii, hati za mirathi zinapatikana katika mahakama hii.
Yeyote anaehusika anatakiwa kuhudhuria mahakama tarehe 17.04.2023 saa 2.00 asubuhi yeye binafsi au wakili wake.
Zingatia kwamba kutokuhudhuria kwenu kwa tarehe tajwa, kesi hii itaendelea kusikilizwa bila ninyi kuwepo mahakamani.
Imetolea kwa mkono wangu na muhuri wa mahakama hii leo tarehe 16/03/2023.

J.A.Mpuya
HAKIMU MKAZI MKUU
MAHAKAMA YA WILAYA NYAMAGANA
MWANZA

PRINCIPAL RESIDENT MAGISTRATE
MWANZA



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**Katika mahakama ya mwanzo ya wilaya ya MISSENYI**
**Kituo cha KANYIGO**
**Mkoa KAGERA**
**Usimamizi wa mirathi Na 03/2023**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU NESTORY YAKOBO wa KIGARAMA**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA**
**NA DIOCLES RUTAKUBANGULA IZOBA**

**TANGAZO**

**(kanuni ya 5(2) ya kanuni za usimamizi wa mirathi Mahakama za mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote wowote/ maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wnaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 19 mwezi 04 mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo

**Zingatia**

Endapo kuna yoyote mwenye wosia wa marehemu anaweza kuuleta mahakamani kukaguliwa
Imetolewa leo tarehe 29 mwezi 03 mwaka 2023

HAKIMU MKAZI MFAWIDHI
MAHAKAMA YA MWANZO
KANYIGO


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BUNGE LA TANZANIA**


Simu: +255 26 2322761-5
Fax No. +255 26 2324218
E-mail: cna@bunge.go.tz

Ofisi ya Bunge
S.L.P. 941
DODOMA.


## TAARIFA KWA UMMA KUHUSU HABARI ZILIZOCHAPISHWA KWENYE GAZETI NA MITANDAO YA KIJAMII KUHUSU KANUNI ZA BUNGE

### 1.0 UTANGULIZI

Gazeti la Mwananchi toleo la Ijumaa tarehe 31 Machi, 2023 liliandika taarifa yenye kichwa cha habari kinachosomeka **"Bunge latunga kanuni mpya kwa wanahabari, wadau wang'aka"**

Katika taarifa hiyo gazeti lilirejea Kanuni za Bunge Toleo la Februari 2023 kwa kudai kuwa Kanuni hizo zimetungwa mwaka 2023. Maudhui ya taarifa hiyo yanalenga kuufahamisha umma kwamba Kanuni hizo zinarudisha nyuma uhuru wa habari kwa kuweka usiri katika shughuli za baadhi ya Kamati. Vilevile alieleza kuwa Kanuni zinaelekeza namna ya kupiga picha Bungeni hivyo kuwanyima uhuru wanahabari. Katika taarifa hiyo inaonekana mwandishi aliwahoji Mwenyekiti wa Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF) Ndugu Deodatus Balile na Mwenyekiti wa Klabu ya Waandishi Habari ya Dodoma Ndugu Mussa Yusuph ambao walitoa maoni kwamba watafanyia kazi taarifa hizo kwa kuchambua Kanuni, kuhoji na kuonana na Uongozi wa Bunge ili kuwezesha kupatikana kwa Kanuni walizodai zitakuwa rafiki kwa waandishi wa habari.

Zaidi ya taarifa hizo, katika mtandao wa kijamii wa Jamii Forums imewekwa taarifa yenye kichwa cha habari **"Bunge lachapisha Kanuni mpya za Bunge zenye masharti kwa Waandishi wa Habari."** Taarifa hiyo imeeleza kuwa Bunge limetunga Kanuni mpya za mwaka 2023 zinazoweka masharti ya adhabu kwa waandishi wa habari na kutoa maelekezo mahsusi ya upigaji picha ndani ya Ukumbi wa Bunge. Taarifa hiyo imefafanua zaidi kwamba licha ya waandishi wa habari kutakiwa kuingiza kamera Bungeni kwa kibali, wakati wa kupiga picha kamera zinatakiwa zielekezwe kwa Spika au Mbunge anayezungumza wakati huo.

### 2.0 MASHARTI KUHUSU UANDISHI WA HABARI BUNGENI

Kanuni zinazosimamia ukusanyaji na utoaji habari Bungeni zimeainishwa katika Nyongeza ya Saba ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Nyongeza hiyo ilikuwepo kwenye Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016. Kutokana na uhitaji, Kanuni hizo zilifanyiwa maboresho ili ziweze kuongoza kwa ufanisi ukusanyaji na utoaji wa taarifa za Bunge. Kufuatia maboresho hayo Bunge lilijadili na kupitisha kwa njia ya Azimio Kanuni za Bunge zilizoitwa Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Juni, 2020. Kabla ya kuanza kutumika, Kanuni hizo zilitangazwa kwenye gazeti la Serikali kupitia Tangazo la Serikali Na. 626 la tarehe 7 Agosti, 2020. Toka wakati huo masharti yanayoongoza waandishi wa habari Bungeni yamekuwa yakizingatiwa ipasavyo ambapo Ofisi ya Bunge haijawahi kupokea maoni wala malalamiko kutoka kwa mtu yeyote ikiwa ni pamoja na wadau wa habari.

### 3.0 KANUNI ZA BUNGE TOLEO LA FEBRUARI, 2023

Mnamo mwezi Februari, 2023 Mheshimiwa Spika kwa kushauriana na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kanuni alifanya marekebisho kwenye Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Juni, 2020. Marekebisho hayo yalilenga kuboresha muundo wa Kamati za Bunge ili kuendana na Wizara za Serikali kwa nia ya kuleta ufanisi katika utendaji kazi wa Kamati. Baada ya marekebisho hayo kufanyika Nyongeza ya Nane ya Kanuni ilitangazwa kwenye gazeti la Serikali kupitia Tangazo la Serikali Na. 37A la tarehe 7 Februari, 2023. Marekebisho hayo yaliunganishwa na Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Juni, 2020. Uunganishaji huo (revision) ulitekelezwa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ambapo Toleo la Februari, 2023 lilipatikana. Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari, 2023 zinatokana na maboresho ya Nyongeza ya Nane inayohusu Kamati za Kudumu za Bunge. Hivyo, hakuna mabadiliko mengine yeyote yaliyofanyika katika Kanuni au Nyongeza nyingine zilizobaki.

### 4.0 UPATIKANAJI WA HABARI ZINAZOHUSU SHUGHULI ZA BUNGE

Nyongeza ya Saba ya Kanuni za Kudumu za Bunge inatoa mwongozo wa kusimamia ukusanyaji na utoaji wa habari za Bunge. Masharti yaliyomo kwenye Nyongeza hiyo yanaruhusu waandishi wa habari kutekeleza wajibu wao ikiwemo kupata habari zinazohusu shughuli mbalimbali za Bunge. Habari hizo zimegawanyika katika sehemu mbili ambazo ni habari za masuala ya kawaida na masuala ya faragha. Masuala ya faragha yamewekewa mipaka na utaratibu wa kuzingatia katika kuzipata na kuzitumia taarifa hizo.

Vilevile Kanuni zimetaja Kamati ambazo vikao vyake vinapaswa kuwa vya siri kuwa ni Kamati ya Uongozi, Kamati ya Kanuni na Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge. Aidha, Kamati nyingine za Bunge zimewekewa masharti ya kufanya vikao vyake kwa siri wakati zinapofanya kazi za kiuchunguzi. Lengo la masharti hayo ni kutoathiri utendaji au matokeo ya kazi zinazofanywa na Kamati hadi pale taarifa zitakapowasilishwa Bungeni. Masharti yanayohusu upatikanaji wa habari za kawaida yametajwa katika Kanuni ya 6 na masuala ya faragha yametajwa katika kanuni ya 7 ya Nyongeza ya Saba ya Kanuni.

Ili kusimamia utekelezaji bora wa shughuli za Bunge, Bunge lilitunga Kanuni ya 4 na 5 za Nyongeza ya Saba ya Kanuni zinazosimamia upigaji picha katika ukumbi na maeneo mengine ya Bunge. Kanuni hizo zimeelekeza utaratibu, namna na makatazo ya upigaji picha Bungeni. Lengo la masharti hayo ni kuhakikisha upigaji picha haungilii shughuli za Bunge.

### 5.0 HITIMISHO

Ni wazi kuwa maelezo ya waandishi kwamba Bunge limetunga Kanuni mpya za Toleo la Februari Mwaka 2023 si sahihi na zinapotosha. Vilevile maoni kuwa Kanuni za Bunge zinawanyima waandishi wa habari fursa ya kupata na kutoa habari siyo sahihi. Kwa mujibu wa Masharti ya Kanuni za Bunge waandishi wanao uhuru wa kupiga picha na kutoa Habari za masuala mbalimbali yanayofanyika kwenye Ukumbi wa Bunge, Kamati zake na kwenye ziara za Kamati. Mambo machache yaliyowekewa masharti ya faragha yanaendana na misingi ya Haki, Kinga na Madaraka ambayo Bunge limepewa Kikatiba na kupitia Sheria ya Haki, Kinga na Madaraka ya Bunge Sura 296.

Kutokana na ufafanuzi wa hapo juu na ili kuepusha kuendelea kusambaa kwa upotoshaji dhidi ya Bunge, tunasisitiza kwamba:-

a) Waandishi wa habari wanao uhuru kutosha wa kuripoti habari za Bunge;

b) Bunge halijatunga Kanuni mpya za Mwaka 2023 kama inavyodaiwa;

c) Kanuni za Bunge zinazotoa mwongozo wa ukusanyaji na utoaji wa habari za Bunge hazijabadilika na zimekuwa zikisimamia eneo hilo kwa ufanisi;

d) Ofisi ya Bunge imekuwa ikishirikiana na wadau mbalimbali wakiwemo wandishi wa habari katika utekelezaji wa shughuli za Bunge. Aidha, Bunge limekuwa likiacha milango wazi ili kupokea maoni na ushauri kwa nia ya kuboresha shughuli za Bunge; na

e) Ofisi ya Bunge inapenda kuwakumbusha waandishi wa habari juu ya umuhimu wa kuzingatia misingi ya uandishi wa habari ikiwemo inayowataka kupata taarifa sahihi kutoka kwa Taasisi husika kabla ya kuchapisha taarifa ili kuepusha upotoshaji na taharuki inayoweza kujitokeza kwa jamii.

Imetolewa na:

**Kitengo cha Mawasiliano na Uhusiano wa Kimataifa;**
**Ofisi ya Bunge;**
**DODOMA.**
**02 Aprili, 2023**



Waziri Mkuu na Mbunge wa Jimbo la Ruangwa, Kassim Majaliwa akimkabidhi Abdulrahman Mnokota moja kati ya pikipiki 100 zenye thamani ya Sh. milioni 250 alizozitoa kwa vijana wa wilaya ya Ruangwa, mkoani Lindi, kwa ajili ya kufanya biashara ya usafirishaji. Kulia ni Mdhamini Mkuu wa pikipiki hizo, Mpaluka Mtopelana. **PICHA: OWM**

# DC: Marufuku kuuza mahindi yakiwa shambani

**Na Gideon Mwakanosya,** SONGEA

MKUU wa Wilaya ya Songea mkoani Ruvuma, Wilman Ndile, amepiga marufuku kwa wafanyabiashara wa ndani na nje kununua mahindi kwa wakulima yakiwa bado shambani hayajakomaa.

Alitoa agizo hilo jana wakati wa uzinduzi wa mbegu bora ya mahindi, ZAMSEED TZ 638, inayozalishwa katika eneo la Ndolela, Halmashauri ya Wilaya ya Madaba.

Ndile aliwaonya wakulima wa wilaya hiyo kuacha tabia ya kuuza mahindi yakiwa shambani kwa walanguzi wanaopita vijijini kuyatafuta.

Alisema msimu uliopita wakulima wilayani humo walipata hasara baada ya baadhi ya wanunuzi waliokuwa wakipita vijijini kununua mahindi kwa kutoa fedha bandia.

Pia, inadaiwa wafanyabiashara hao kutoka mikoa ya Dar es Salaam, Mtwara, Arusha na Kenya walipita vijijini kuwarubuni wakulima ili wawauzie mahindi kwa bei ndogo ambayo hailingani na gharama za uzalishaji kwa zao hilo.

Alisema hali hiyo ni kero kwai sasa kwa kuwa wakulima waliuza mahindi yote bila kuacha akiba ya chakula na kuwasababishia kukosa akiba ya familia zao.

Kutokana na hali hiyo, aliwagiza viongozi wa serikali za vijiji, kata, wakurugenzi wa halmashauri za wilaya hiyo wahakikishe wanawadhibiti wafanyabiashara wanaokwenda kununua mahindi kwa wakulima na badala yake wafuate utaratibu.

Ndile alisema katika msimu ujao serikali imejipanga kununua mahindi ya wakulima kwa bei nzuri kupitia kwa Wakala wa Hifadhi ya Taifa ya Chakula (NFRA) Kanda ya Songea na Bodi ya Mazao Mchanganyiko (CPB).

Alifafanua kuwa CPB imeshatenga Sh. bilioni 100 kwa ajili ya kununua mahindi kwa wakulima na kuwataka waone umuhimu wa kutokuhangaika kuuza bila kufuata taratibu zilizowekwa na serikali.

Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni ya ZAMSEED TZ, Frank Kileo, aliwataka wakulima wa mikoa ya Ruvuma na Njombe kuitumia mbegu hizo zinazozalishwa mkoani Ruvuma kwa vile zina uwezo mkubwa wa uzalishaji wa mahindi na kuhimili ukame pamoa na mvua nyingi.

Alifafanua kuwa mbegu hizo zimefanyiwa utafiti wa kutosha na zina uwezo wa kuzalisha mpaka magunia 40 kwa ekari moja endapo mkulima atafuata taratibu zote za kilimo bora.

# Waziri Mkuu akabidhi vijana pikipiki 100

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa amekabidhi pikipiki 100 zenye thamani ya Sh. milioni 260 kwa vijana wa Wilaya ya Ruangwa ili wazitumie kufanya biashara ya usafirishaji.

Akizungumza na vijana hao kwenye hafla ya kukabidhi pikipiki hizo iliyofanyika mwishoni mwa wiki kwenye viwanja vya CWT, wilayani Ruangwa mkoani Lindi, Waziri Mkuu alisema utoaji wa pikipiki hizo ni mwendelezo wa mpango wa ofisi ya Mbunge wa kuwawezesha vijana, wanaume, wanawake na wazee.

"Mwaka 2016/2017 tulichukua pikipiki 235 na kuzigawa kwenye wilaya yote hii. Na jambo zuri kwa sasa, kwenye Serikali ya awamu ya sita, Mheshimiwa Dk. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Tanzania na yeye ameamua kuwa na kada ya wasafirishaji wadogo, wa kati na wakubwa."

Majaliwa ambaye pia ni Mbunge wa Ruangwa aliwataka vijana watambue kwamba na wao ni wasafirishaji wa usafiri wa kawaida kwa kutumia pikipiki.

Akielezea mradi huo, Mwenyekiti wa wafanyabiashara wadogo wa soko la Kariakoo, jijini Dar es Salaam, Martin Mbwana, alisema pikipiki hizo zitakopeshwa kwa bei ya Sh. milioni 2.6 bila riba na muda wa marejesho ni miezi minane.

"Kuanzia sasa hadi Desemba, mwaka huu mtu anapaswa awe amekamilisha mkopo wake. Na kianzio ni kati ya Sh. 500,000 hadi 700,000. Mkopo huu umetolewa chini ya mdhamini mkuu, Mpaluka Hashim Mtopela," alisema.

Alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kufungua milango ya biashara na kuongeza: "Nikiwa mwenyekiti wa wafanyabiashara wadogo wa soko la Kariakoo, niko hapa Ruangwa ili kuwawezesha vijana wa Ruangwa," alisema.

Mtopela alimshuruku Waziri Mkuu kwa kuamua kuwajali vijana wa jimbo lake. "Mwaka 2016 ulitoa pikipiki 235 ambazo zimewesha vijana zaidi ya 600 kuishi maisha mazuri wao na familia zao. Wako waliopewa pikipiki moja, lakini leo hii wanamiliki pikipiki tatu hadi nne." "Hii ina maana leo tukimpa kijana sh. milioni 2.6, baada ya muda ataweza kutengeneza shilingi milioni saba. Vijana hawa nimewachukulia dhamana kwa sababu ninaamini wanaweza kuzirejesha. Safari hii tumechukua pikipiki, lakini muda ujao tutachukua mashine ya kufyatulia matofali au ya kumwagilia bustani kwa sababu tunao vijana wenye uwezo," alisema.

# TFS yahofu ongezeko mifugo kuingia misitu ya hifadhi

**Na Beatrice Shayo, RUFIJI**

MHIFADHI Mkuu wa Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), Wilaya ya Rufiji mkoani Pwani, Francis Kiondo, amesema kumekuwa na ongezeko kubwa la mifugo inayoingizwa ndani ya misitu ya hifadhi hali inayosababisha uharibifu wa mazingira.

Kiondo aliyasema hayo jana kwenye maadhimisho ya siku ya upandaji miti kwenye hifadhi ya majimoto chemchem iliyopo Utete, Wilaya ya Rufiji eneo hilo limepandwa miti 1,000 na kufikia idadi ya 134,700 iliyopandwa lengo ni kupanda miti milioni 1.5 kwa wilaya, kila mwaka.

Alisema licha ya jitihada mbalimbali zinazofanywa na serikali katika kuinusuru misitu ya wilaya isiangamie, kumekuwa na changamoto zinazojitokeza kila siku ikiwamo mifugo kuingizwa kwenye misitu ya hifadhi kinyume cha sheria.

Kiondo alisema kuna tatizo la uelewa mdogo wa manufaa ya faida zitokanazo na misitu.

Alisema kumekuwa na kilimo kikubwa cha kuhamahama katika maeneo ya mtaji wazi na ardhi za vijijini pamoja na uvamizi kwenye hifadhi za misitu. "Uvamizi wa maeneo ya vyanzo vya maji na kufanya shughuli za kibinadamu kama vile kilimo na uvuvi," alisema Kiondo.

Aidha, alisema hatua mbalimbali zimechukuliwa ili kupambana na changamoto hizo ikiwamo kutoa elimu ya uhifadhi na utunzaji wa mazingira kwa jamii hususani maeneo yenye uvunaji, kwenye shule na wafanyabiashara na wavunaji wa rasilimali zitokanazo na misitu.

Ofisa Mtendaji wa Kata ya Chemchem, Wilaya ya Rufiji, Jonathan Chingwile, akisoma hotuba ya Mkuu wa Wilaya ya Rufiji, Meja Edward Gowele, alisema miti ni rasilimali muhimu katika maisha ya binadamu, hivyo ni muhimu wananchi wakaelewa.

Alisema miti husaidia upatikanaji wa mvua, hupunguza hewa ya ukaa, hutunza ardhi, hutoa hewa safi ya oksijeni na mazao ya miti mbao, mkaa na kuni. Hata hivyo, alisema jamii zinatoa umuhimu mdogo wa kupanda na kutunza miti katika wilaya ndio maana ikawekwa siku ya upandaji miti kitaifa na wilaya ili kuwakumbusha suala muhimu la kutunza na kuwekeza kwenye rasilimali za miti.

Alisema Wilaya ya Rufiji imejaliwa kuwa eneo kubwa la ardhi ambalo linafaa kwa upandaji ingawa suala hilo linakwenda kwa kusuasua.

Aidha, alisema kumekuwa na matukio ya uchomaji miti ovyo, ukataji miti kwa ajili ya shughuli mbalimbali za kijamii ikiwamo kilimo na uvunaji wa miti bila kufuata sheria.

Alisema changamoto ambazo zinaathiri misitu na tahadhari zisipochukuliwa zitasababisha wilaya kukumbwa na tatizo la upungufu wa mvua hali inayosababisha ukame wa muda mrefu na kugeuka jangwa hapo baadaye.

# Mfanyabiashara mbaroni kukutwa chakula cha ruzuku

**Na Said Hamdani, LINDI**

JESHI la Polisi mkoani Lindi linamshikilia mfanyabiashara, Mohamed Seif (50), kwa tuhuma za kukutwa na magunia 62 ya mahindi ya ruzuku yaliyotolewa na serikali kwa ajili ya kuwauzia wananchi kwa bei nafuu.

Kamanda wa Polisi mkoani humo, Pili Mande, alitoa taarifa hiyo wakati akiwasilisha taarifa ya uwajibikaji kwa kipindi cha miezi mitatu kuanzia Januari hadi Machi, mwaka huu.

Alisema mfanyabiashara huyo alikamatwa na kiasi hicho cha mahindi yenye uzito wa kilo 3,200, baada ya msako.

Kamanda Mande alisema mfanyabiashara huyo alikamatwa Machi 25, mwaka huu akiwa na magunia hayo yaliyokuwa yamehifadhiwa kwenye viroba vya uzito wa kilo 50 yakiwa na nembo ya NFRA pamoja na magunia matupu 100 yaliyokuwa yamehifadhiwa nyumbani kwa Msomanga. Alisema kwa sasa mfanyabiashara huyo anaendelea kushikiliwa kwa upelelezi kutambua alivyoyapata mahindi hayo na baada ya kukamilika watamfikisha mahakamani kujibu tuhuma hizo.

"Kwa sasa huyu mfanyabiashara tunaendelea na upelelezi wetu, baada ya kukamilisha tutamfikisha kunakohusika kujibu tuhuma zake," alisema Kamanda Mande.

Aliwataka wafanyabiashara wote mkoani Lindi kutojihusisha na vitendo vinavyoweza kuwaletea matatizo ili kulinda heshima na biashara zao na kwamba serikali ipo macho kukabiliana na vitendo viovu.



Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya Biashara Tanzania, Sabasaba Moshingi (katikati), akizungumza na viongozi wa Tigo, kuhusu fursa za biashara na ushirikiano baina ya taasisi hizo mbili, walipotembelea katika makao makuu ya benki hiyo, Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# 'SUK' imesaidia kuimarisha demokrasia Z'bar'

**Na Mwandishi Wetu**

CHAMA cha Mapinduzi (CCM) Zanzibar, kimesema Serikali ya Umoja wa Kitaifa imesaidia kuimarisha misingi ya demokrasia na umoja wa kitaifa kwa wananchi wa Zanzibar.

Katibu wa Idara ya Itikadi, Uenezi na Habari, Khamis Mbeto Khamis, alisema hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari Hospitali ya Al- Rahma kumjulia hali aliyekuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Maridhiano, Ali Mzee Ali, aliyelazwa katika hospitali hiyo.

Alisema tangu kufanyika kwa marekebisho ya 10 ya Katiba ya mwaka 1984 na baadaye kuundwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa, siasa za chuki zimetoweka na misingi ya umoja wa kitaifa ikiendelea kuimarika visiwani humo.

Alisema, Zanzibar sasa inashuhudia siasa za kistaarabu kwa wanachama na vyama vya siasa vikishindana na kukosoana kwa hoja badala ya siasa za chuki na uhasama.

"Sote mashahidi tunashuhudia siasa za kistaarabu zikiendelea kuimarika Zanzibar huku siasa za chuki na uhasama zikibakia historia katika siasa za Zanzibar na haya ni matunda ya uwapo wa serikali ya umoja wa kitaifa," alisema.

Aidha, alisema miradi ya maendeleo inayoendelea kujitokeza Zanzibar katika sekta ya elimu, afya, miundombinu na sekta zingine, imetokana na kuimarika kwa hali ya amani na usalama nchini.

Alisema, wananchi wanapaswa kuheshimu na kuenzi serikali hiyo ambayo ni chimbuko la amani inayoendelea kutawala visiwani humo tofauti na miaka ya nyuma baada ya kuanzishwa kwa mfumo wa vyama vingi.

Akizungumza hospitalini hapo, mwanasiasa huyo mkongwe Ali alisema anaendelea vizuri baada ya kupatiwa matibabu tangu alipolazwa Machi 25, mwaka huu.

"Hali yangu inaendelea kuimarika tangu nilipoanza kupatiwa matibabu, nawashukuru kwa kufika kunijulia hali wakiwamo viongozi wa kitaifa," alisema Mzee.

Mfanyabiashara maarufu visiwani Zanzibar na kada wa CCM, Saleh Mohamed Said, alisema amefika kumjulia hali mwanasiasa huyo baada ya kupokea taarifa kuwa amelazwa hosptali akisumbuliwa na matatizo ya kiafya.

Aidha, alisema amefarijika kuona hali yake ya kiafya ikiendelea kuimarika na kumuomba Mungu aendelee kumpa nguvu na kumuondolea maradhi yanayomsumbua.

Viongozi wingine waliofika kumjulia hali mwanasiasa huyo ni Rais mstaafu wa Zanzibar, Dk. Amani Abeid Karume, Rais mstaafu Dk Ali Mohamed Shein, Makamu wa Kwanza wa Rais, Othman Masoud Othman, aliyekuwa Naibu waziri Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Mihayo Juma Nhunga, Kamishna wa Polisi Zanzibar, Hamad Khamis Hamad na mshauri wa Chama cha ACT-Wazalendo, Mansour Yussuf Himid.

Tangu kulazwa kwa mwanasiasa huyo viongozi wa kitaifa, wanasiasa na wanaharakati wamekuwa wakipishana katika ngazi za jengo la hospitali hiyo kumjulia hali mwanasiasa huyo.

# 'Uchafuzi fukwe za bahari wahatarisha viumbe hai'

**Na Elizabeth Zaya**

TAASISI ya Rotary Club ya Mbezi Beach kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imesema uchafuzi wa mazingira unaofanywa katika fukwe za bahari unahatarisha vifo vya viumbe hai na kuharibu ikolojia ya mazingira.

Ilisema hayo walipofanya usafi katika fukwe ya bahari ya Mtaa wa Mbezi Beach, Shina namba saba, jijini Dar es Salaam wakishirikiana na wananchi wa mtaa huo, NAK limited, taasisi ya The Recycler, WFO, Blue Courses na Kampuni ya uzalishaji saruji ya Twiga Cement.

Rais mstaafu wa Rotary Club ya Mbezi Beach na Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya NAK Limited, Pamela Mutabazi, alisema lengo la kuamua kufanya usafi katika fukwe hiyo ni baada ya kubaini uchafuzi mkubwa katika fukwe hiyo.

"Fukwe ni kivutio cha utalii, kwa hiyo zikiwa safi ndipo zinavutia watu wengi kuja na kufanya shughuli zao mbalimbali na wanapokuja wanasaidia pia kuwapa wengine kipato au ajira kwa sababu ni lazima wafurahi kwa kula na kunywa na ndio maana sisi kama wadau wa mazingira tukaamua kuja kuhamasisha namna ya kuzisafisha na kuzitunza," alisema Pamela.

"Na tumeshuhudia hapa namna Mto Mbezi unavyochangia uchafuzi wa mazingira katika fukwe hii ya Mbezi Beach, kwa hiyo ndio maana tuliona tubuni hii kampeni ya usafi endelevu ambayo tunaamini itatatua tatizo hili na tumewashirikisha wananchi wa eneo hili."

Aliwaomba wananchi kutowafumbia macho wanapobaini kuwapo kwa watu wanaochangia au kufanya uchafuzi huo wa mazingira katika fukwe yao na kwamba watahakikisha kazi hiyo ya usafi katika fukwe inafanyika kila mwezi.

Philip Stephen wa Kampuni ya The Recycler alisema uchafuzi wa mazingira kwenye fukwe, ardhi, vyanzo vya maji vyote kwa pamoja vina athari kubwa, ni vema jamii ikachukua hatua kudhibiti.

"Suala la usafi wa mazingira ni la kila mtu kwa kujua kwamba kufanya hivyo kunaleta faida kwenye mazingira na afya zao na kunapunguza vifo ambavyo hutokana na uchafuzi huo wa mazingira."

Mjumbe Msaidizi wa Serikali ya Mtaa wa Mbezi Beach Shina namba saba, Joyce Masawe, alisema wakazi wa eneo hilo wamekuwa wakipata athari mbalimbali zinazosababishwa na uchafuzi wa fukwe hiyo hususani harufu mbaya inayotokana na uchafu unaotupwa katika eneo hilo.

"Huu Mto Mbezi umekuwa ukitiririsha uchafu mwingi katika eneo letu hili la fukwe, hapa utaona sindano zilizotumika, chupa za bia, za soda, makopo, uchafu tofauti wa hospitalini, na hivi vyote huwa vinakuja kupasukia hapa. Hii ni hatari kwa sababu vinaweza kuwaumiza hata waogeleaji na hata sisi wengine tunaathirika na harufu mbaya," alisema Joyce.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Simba, Yanga anzeni sasa maandalizi robo fainali CAF

**DROO** ya robo fainali ya michuano ya Ligi ya Mabingwa na Kombe la Shirikisho barani Afrika, inatarajiwa kufanyika keshokutwa, Jumatano jijini Cairo, Misri yalipo makao makuu ya Shirikisho la Soka Afrika, CAF.

Hii itakuwa mara ya kwanza katika historia ya michuano hiyo kwa droo hiyo kufanyika ikizihusisha timu mbili kutoka Tanzania, Simba na Yanga, ambazo zote zimefuzu hatua ya mashindano hayo yenye utajiri mkubwa kwa ngazi ya klabu barani Afrika.

Klabu hizo kongwe nchini, Simba imefuzu hatua hiyo kwa upande wa Ligi ya Mabingwa wakati watani zao, Yanga wakitinga hatua hiyo kwenye kinyang'anyiro cha Kombe la Shirikisho Afrika ambayo ni michuano ya pili kwa utajiri barani humu kwa ngazi ya klabu baada ya hiyo ya Ligi ya Mabingwa.

Baada ya kazi kubwa na ngumu, klabu hizo ilizofanya katika hatua ya makundi, sasa zinaelekea kugumu zaidi ambayo inachezwa kwa mtindo wa mtoano, hivyo zinapaswa kufanya maandalizi makubwa zaidi ili kuweza kuendelea kuipeperusha vema bendera ya nchi katika michuano hiyo inayoandaliwa na kuratibiwa na CAF.

Tunaamini kama Simba na Yanga zitarekebisha makosa madogo madogo yaliyojitokeza katika mechi zao za hatua ya makundi hususan katika kutumia vema nafasi wanazotengeneza na kwenye kujilinda, zinaweza kabisa kuvuka robo fainali na kutinga nusu fainali na hatimaye fainali.

Na hilo ndilo tunalotamani kuona likitokea na hatimaye kutwaa ubingwa huo, lakini halitaweza kuja kwa kuzungumza tu pasipo wachezaji, mabenchi ya ufundi, viongozi hadi mashabiki, kila mmoja kwa nafasi yake kujitoa vilivyo kuzisapoti timu zao kwa namna moja ama nyingine.

Tulishuhudia mechi za mwisho timu hizo kucheza nyumbani namna ambavyo mashabiki waliitika wito wa viongozi wa klabu hizo, kwa kujitokeza kwa wingi uwanjani kuzishangilia mwanzo mwisho wa mchezo, hiyo ikionyesha matamanio walio nayo kuona zinafika mbali zaidi.

Kwa mantiki hiyo, katika kipindi hichi kuelekea mechi hizo za robo fainali, ni wakati wa kila mchezaji kujituma vilivyo mazoezini na kusikiliza vema maelekezo ya makocha wao, ili kuweza kupata matokeo chanya yatakayowawezesha kutinga hatua inayofuata.

Ingawa kadri michuano hiyo inavyosonga mbele ndivyo inavyokuwa migumu zaidi, tunaamini hakuna linaloshindikana endapo kila mchezaji atalibeba jukumu hili kama daraja lake la mafanikio la kukitangaza kipaji chake, lakini pia kuongeza sifa zaidi katika wasifu wake kisoka.

Hii ni kutokana na hatua kama hii ya michuano hiyo mikubwa kwa ngazi ya klabu barani Afrika, ndiyo ambayo mawakala wengi hutupia jicho zaidi ili kupata wachezaji watakaowauza Ulaya, Asia na kwingineko kulikopiga hatua kisoka, hivyo kila mchezaji hana budi kutambua kwamba haipigania nembo ya klabu pekee bali pia ni fursa adhimu katika kulitangaza soka lake kimataifa.

Kwa kulitambua hilo, ni matarajio yetu kuwa kila mmoja atajituma vema katika kuhakikisha klabu yake inaandika tena rekodi kwa kutinga hatua ya nusu fainali na hatimaye fainali kama si kubeba mataji hayo kwa msimu huu.

Hayo ndiyo mafanikio tunayoyataka, ambayo yatakwenda kulitangaza soka letu na lao pia, hivyo kuongeza thamani ya Ligi Kuu Tanzania Bara jambo litakalovutia wawekezaji wengi na hata mawakala kuifuatilia kwa karibu.

Lengo letu si tu kuona Simba na Yanga zikifika mbali kwenye michuano hiyo, bali kuwa daraja la wachezaji kupata klabu kubwa nje ya nchi na kwenda kucheza soka la kulipwa ili kujiongezea kipato chao kwa kuwa tunatambua soka ni ajira na wanaishi kwa kupitia vipaji vyao uwanjani.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Adam Fungamwango

## Muungwana Lazima Nilonge

# Ligi Kuu inarejea hatutaki tena visingizio

**KUANZIA** Ijumaa ijayo Ligi Kuu Tanzania Bara itarejea baada ya kusimama kwa muda kupisha mechi za kimataifa. Ligi ilisimama tangu Machi 13, mwaka huu kupisha mechi za Ligi ya Mabingwa Afrika, Kombe la Shirikisho na mechi za kusaka tiketi ya Fainali za Mataifa ya Afrika (Afcon) 2023, zinazotarajiwa kufanyika mapema mwakani nchini Ivory Coast.

Hii itakuwa ngwe ya mwisho ambapo timu zinaenda kusaka ubingwa, zingine zikitafuta nafasi ya kucheza mechi za kimataifa msimu ujao, zipo pia zinazosaka pointi ili ziwe maeneo salama na zile zinazopigana kufa au kupona kuepuka janga la kushuka daraja.

Kwa haraka haraka tu, ukiangalia hata msimamo wa ligi itaona kabisa timu zimejigawa katika makundi manne. Timu zinazowania ubingwa mpaka sasa ni mbili tu, Simba na Yanga, zingine zote zimeshanyoosha mikono juu. Halafu kuna vita ya Singida Big Stars na Azam FC kwenye kuwania nafasi ya tatu na ya nne kusaka nafasi ya kucheza michuano ya kimataifa mwakani.

Yeyote kati ya hiyo itakayoshika nafasi ya tatu kwenye Ligi Kuu, moja kwa moja itacheza Kombe la Shirikisho barani Afrika, lakini itakayoshika nafasi ya nne bado itakuwa haina uhakika.

Itasubiri bingwa wa Kombe la FA iwe timu ambayo inashika nafasi tatu za juu kwenye Ligi Kuu, hapo ndipo nafasi ya nne itakapokuwa na umuhimu, haitokuwa na umuhimu wowote, ndiyo maana Azam na Singida Big Stars wanapigana vikumbo.

Kuna timu za Geita Gold, Ihefu, Namungo na Kagera Sugar hizi kwa pointi zilizo nazo ni kama zinajazia tu kwani zinaonekana zipo eneo salama na hazina shaka msimu ujao tukaziona tena kwenye Ligi Kuu.

Lakini timu za Polisi Tanzania, Ruvu Shooting, Prisons, Coastal Union, KMC, Dodoma Jiji, Mbeya City na Mtibwa Sugar bado hazipo salama kwani kati ya hizi, mbili zitashuka daraja na mbili zinakwenda kucheza mechi za mchujo na timu za Ligi ya Championship.

Kutokana na mazingira haya, tunatarajia kuona kivumbi kwenye mechi za kumalizia ligi ya msimu wa 2022/23, timu zikipambana kila moja ikihitaji inachokitaka.

Ni kipindi ambacho waamuzi wanatakiwa kuwa makini kwani wanabeba mustakabali wa klabu hizo kwa sababu tumeshuhudia baadhi ya timu zimeshuka, lakini hazijaweza kurejea tena Ligi Kuu. Kwa hiyo kuishusha kwa kuionea kwa sababu zozote zile haitoleta picha nzuri wala kulisaidia soka la nchi.

Kwa kipindi ambacho ligi inachezwa tumekuwa tukisikia baadhi ya makocha wa timu zinazoitwa au kujiita ndogo wakilalamika uchovu wa wachezaji wao kutokana na kucheza mechi mfululizo pamoja na kusafiri, wakidai timu kubwa zenyewe zimekuwa na uwezo wa kusafiri kwa ndege.

Makocha wengine wakawa wanajifichia kwenye kivuli hicho, wakisema ubora wa wachezaji wao hauonekani kwa sababu wachezaji hawapumziki.

Kwa kipindi hiki naweza kusema ni wachezaji wachache sana waliokuwa wakiendelea kucheza, lakini wengi walikuwa mapumzikoni, hivyo haitokuwa tena sababu.

Wachezaji walioonekana kutopumzika wengi wao ni wa Simba na Yanga ambao walikuwa wakicheza mechi za kimataifa na kuunganisha kwenda kuzichezea timu zao za taifa. Wachache tu ni wa timu zingine.

Sidhani sasa kama baadhi ya makocha watajificha kwenye kichaka hiki kwa sababu wakati wenzao wanaendelea kucheza mechi za kimataifa, wachezaji wa timu zao walipumzika. Kwa mujibu wa makocha wenyewe alipohojiwa, wachezaji wao walipumzika zaidi ya siku 10 kabla ya kurejea tena mazoezini kujiandaa na ligi, zingine zikipata pia mechi za kirafiki.

Tunataka timu zipambane na timu ikishindwa makocha watupe sababu za kiufundi na si uchovu tena wa safari au wa kucheza mechi mfululizo.

## Serikali yaipongeza AMF kuwatambua wenye mahitaji

**Na Maulid Mmbaga**

KATIBU Mkuu Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto, Zanzibar Abeida Rashid Abdallah ameipongeza Taasisi ya Asma Mwinyi Foundation (AMF) kwa kuwatambua na kushughulikia watoto wenye mahitaji maalum.

Aliyasema hayo jana Mkoa wa Mjini Magharibi, wakati wa futari maalum iliyoandaliwa na taasisi hiyo kwa ajili ya watoto wanaoishi katika mazingira magumu.

Alisema kitendo hicho ni cha kiungwana kwa kuwa kinasaidia serikali utekelezaji wa majukumu ya kuwawezesha watoto wenye mahitaji maalum.

"Kuwapo kwa taasisi kama hii inatusaidia sana sisi serikali kwa makundi ya watoto wenye mazingira magumu hivyo ninamuomba Mkurugenzi wa AMF, Asma Mwinyi, aendelee na moyo huu na ninamuahidi kuwa nikiwa kama Katibu Mkuu ninayeshughulikia wizara hii tutashirikiana naye kwa kuwasaidia watoto hawa," alisema.

Alisema Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, itaendelea kumuunga mkono muasisi huyo wa AMF kuwasaidia watoto wanaoishi kwenye mazingira magumu ili wanapate mahitaji yao kama watoto wengine.

"Katika kipindi hiki cha Mwezi Mtukufu wa Ramadhani tunaomba taasisi zingine zimuunge mkono Asma Mwinyi Foundation katika kuwasaidia watoto hawa ili nao waishi kwenye mazingira mazuri," alishauri.

Naye Mkurugenzi wa taasisi hiyo, Asma alisema madhumuni ya kuandaa futari kwa watoto wenye mahitaji maalum katika kipindi hiki cha mwezi Mtukufu wa Ramadhani ni kuwakutanisha pamoja na kuwafariji.

"Tumewakutanisha watoto ambao wanaishi pia kwenye mazingira magumu wakiwamo wasiokuwa na wazazi na wenye ulemavu wa ngozi, leo 'jana' tumeona tuwatoe katika mazingira ambayo wanaishi na tuwalete sehemu ya tofauti ili wajisikie tofauti," alisema.

**Alisema kitendo hicho ni cha kiungwana kwa kuwa kinasaidia serikali utekelezaji wa majukumu ya kuwawezesha watoto wenye mahitaji maalum.**



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji Zanzibar, Mudrick Soraga (wapili kushoto) na Ofisa Mkuu wa Uendeshaji Benki ya CRDB, Bruce Mwile (wa nne kulia), wakikabidhi msaada wa futari kwa vituo vya kulelea watoto vya Jukumakhe cha Melitano na Sebleni Masjid Jumma, wakati wa hafla ya futari iliyoandaliwa na Benki ya CRDB jijini Zanzibar mwishoni mwa wiki. Wengine ni Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi Jimbo la Kikwajuni, Nassoro Salim Ali (wapili kulia), Ofisa Mkuu wa Fedha wa benki hiyo, Fredricck Nshekanabo (kushoto) na Mkuu wa Kitengo cha CRDB Al Barakah, Rasid Rashid (kulia). **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

# RITA kutoa huduma zote kidijitali

**Na Joseph Mwendapole,**
MOROGORO

WAKALA wa Usajili Ufilisi na Udhamini (RITA), umetambulisha mfumo mpya wa kutoa huduma zake zote kidijitali unaofahamika kama e-RITA.

Mfumo huo ulitambulishwa mwishoni mwa wiki mkoani Morogoro na Kabidhi Wasihi Mkuu wa RITA, Angela Kemanzi, wakati wa mjadala wa kazi za wakala kwenye mkutano wa 12 wa wanachama wa Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF).

Alisema mfumo huo ni maboresho muhimu na ya msingi ambayo yanakwenda kuleta mapinduzi makubwa katika kupanua wigo wa kuwafikia wananchi wengi wa maeneo ya vijijini na mijini.

Alisema waliamua kushirikisha vyombo vya habari katika hatua za awali za mfumo huo kwa kuwa ni wadau muhimu na daraja baina ya RITA na wananchi wanaowahudumia.

"Tumeona tuzungumze na nyinyi kabla hata ya uzinduzi utakaofanyika hivi karibuni ili mtusaidie kujenga taswira chanya kwa umma na kukuza imani kwa wananchi ambao sisi tumepewa dhamana ya kuwatumikia. RITA na TEF ni wadau muhimu na tutaendelea kushirikiana," alisema.

Alisema mwaka 2017, RITA ilitutaka na wanachama wa TEF kuwapa elimu kuhusu maboresho ya usajili wa matukio muhimu ya binadamu Afrika, Tanzania ikiwa moja wapo na hususan mpango wa kusajili watoto chini ya miaka mitano.

Alisema mpaka sasa kwa miaka 10 mpango huo umefanywa kwenye mikoa 23 na matokeo yamekuwa mazuri kwa kuwa kwa kipindi hicho watoto milioni nane wamesajiliwa na kupewa vyeti.

Alisema walitarajia kukamilisha mpango huo mwaka huu, lakini changamoto zilijitokeza na kubaki mikoa ya Dar es Salaam, Kigoma na Kagera, mikakati waliyojiwekea wanatarajia kuikamilisha mwaka 2024.

"Ni mpango endelevu tunashukuru mliupokea na kuzungumza na jamii ya watanzania changamoto huwa hazikosekani kwa jambo lolote jipya ila ni mpango ambao umetuletea matokeo makubwa na tukienda kwenye vikao kwa wenzetu Afrika tunasifiwa kwa kufanikisha mpango huu," alisema.

Alisema Tanzania imejitahidi kwa kuhakikisha ndani ya kipindi cha miaka 10 imepiga hatua na kusajili idadi kubwa ya watoto, haikuwa kazi nyepesi kupata mafanikio hayo.

Ili kufikia mafanikio hayo, RITA inafanyakazi na wadau mbalimbali nchini na aliwashukuru kwa ushirikiano walioutoa na kuhakikisha idadi kubwa ya watoto inasajiliwa.

Pia, serikali kupitia RITA ina programu mbalimbali zinazolenga makundi mengi kama programu inayoitwa six to seventeen (6/17) ambayo inawalenga watoto walio shule ya msingi na sekondari na vyuoni.

"Hao nao wanasajiliwa kupitia kampeni mbalimbali na tumeendelea na maboresho lakini sasa tumekuja na huu mfumo wa e RITA ambayo ni maboresho ya kidijitali kumwezesha mwananchi kuomba huduma palepale alipo bila kulazimika kwenda ofisi ya RITA, atalazimika kufika kwenye kituo atakachochagua yeye kwaajili ya kupokea cheti chake," alisema.

Alisema wataalamu wa wakala kwa kushirikiana na wengine wa serikali wameendelea kuutengeneza na kuuboresha mfumo huo na sasa wako tayari kuuzindua kwa mapana.

Alitaja huduma zitakazopatikana kwenye mfumo huo kuwa ni za vizazi vifo, udhamini na ndoa na kwamba wataalamu wanaendelea na jitihada ili kuongeza huduma zaidi kwenye mfumo huo.

"Udhamini nayo ni huduma pana sana kuna wale wanaoomba kwa mara ya kwanza kuna wale wanaoomba kwa mara ya pili wale wanaotaka uhakiki, ndoa ina mambo mengi pia wale wanaoomba leseni wale wanaotaka vyeti kwa hiyo katika hizi huduma zinazopatikana kwenye mitandao zina vipengele vingi ambavyo tutaendelea kuvipandisha kwenye mfumo," alisema.

Alitaja moja ya changamoto kubwa wananchi kukosa huduma za RITA ni umbali na muda, lakini kwa kutumia mfumo wa eRITA mwananchi atakamilisha maombi yake na kupata huduma bila kwenda mwenyewe kwenye ofisi za wakala.

## KABWELA

FADHILI MOHAMED



# Machinjio ya kisasa PSSSF yauza nyama nje

**Na Joseph Mwendapole,** MOROGORO

KIWANDA cha nyama cha Nguru Hills Ranch, Morogoro chenye machinjio ya kimataifa, kimeanza kusafirisha nyama nje ya nchi na kimepata soko kubwa nchi za Uarabuni.

Kiwanda hicho kinamilikiwa kwa ubia na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF) yenye asilimia 39 ya hisa, Eclipse ya nchini Oman yenye asilimia 46 na busara yenye asilimia 15.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki na Meneja wa kiwanda hicho, Erick Cormack, wakati wanachama wa Jukwaa la Wahariri (TEF), walipotembelea kiwanda hicho mwishoni mwa wiki.

Alisema ranchi yao iliyoko Wilaya ya Mvomero, Wilaya ya Morogoro ina uwezo wa kuhifadhi ng'ombe 10,000 na mbuzi 15,000 kwa wakati mmoja.

Alisema machinjio ina uwezo wa kuchinja ng'ombe 100 na mbuzi 1,000 kwa siku na asilimia 80 ya nyama inayozalishwa kwenye machinjio hiyo inasafirishwa nje ya nchi na asilimia 20 inauzwa kwenye soko la ndani.

Alisema soko kubwa la nyama ya machinjio yao ni Qatar, Oman Bahrain, United Arab Emirates (UAE), Kuwait, Saudi Arabia, Malasyia, Indonesia na China.

"Nyama yetu inakidhi viwango vya kimataifa kwasababu tumeshaanza kuuza kwenye masoko hayo kwa wingi kuanzia mwaka jana imepokewa vizuri na inaweza kushindana na nyama inayotoka kwenye nchi mbalimbali duniani," alisema.

Alisema wamesajili watu waliozunguka nchi nzima kwaajili ya kununua ng'ombe wa kunenepeshwa kwenye ranchi hiyo kabla ya kuchinjwa.

Alisema, ng'ombe akishafikishwa kwenye ranchi hiyo anakaa miezi mitatu akinenepeshwa kwa virutubisho mbalimbali na baada ya hapo akikidhi vigezo ndipo huchinjwa.

Miradi mingine ambayo PSSSF inaifanya kwa ubia ni Kiwanda cha Chai cha Mponde Tea Tanga, Karanga International Leather Industries Limited kilichopo Moshi, Kilimanjaro na Mamba Miamba Ginger kilichoko Same mkoani Kilimanjaro.




Meneja wa Benki ya Biashara Tanzania (TCB) Tawi la Nzega, Shomari Shabani, (mwenye koti jeusi), akiwa na Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Nyasa pamoja na maofisa wa benki hiyo na wanafunzi, baada ya kukabidhi msaada wa madawati 70 kwa shule hiyo, wilayani Nzega, mkoani Tabora mwishoni mwa wiki ikiwa ni sehemu ya kampeni TCB kuunga mkono juhudi katika sekta ya elimu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## TCB yatoa msaada madawati Shule ya Msingi Nyasa

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya TCB imetoa msaada wa madawati 70 kwa Shule ya Msingi Nyasa, iliyopo Wilaya ya Nzega mkoani Tabora, ikiwa ni mwendelezo wa kuiunga mkono serikali kuboresha ubora wa elimu nchini.

Akizungumza kwenye hafla ya kukabidhi madawati hayo iliyofanyika kwenye viwanja vya shule hiyo mwishoni mwa wiki iliyopita, Meneja wa TCB Nzega, Shomari Shabani, alisema msaada huo ni sehemu ya jitihada inazofanya kusaidia jamii inayoizunguka.

Shabani alisema benki hiyo imekuwa ikijiweka mstari wa mbele kushirikiana na serikali ili kufanikisha mipango mbalimbali katika kuboresha sekta ya elimu, afya, hatua inayosababisha kuwa chachu ya maendeleo kwa sekta zote.

"Mchango uliotolewa na TCB wa kuchangia katika elimu unatokana na matumaini yetu kuwa bila kuwa na jamii iliyoelimika hata huduma za kibenki tunazozitoa zitadhoofika kutokana na ukweli kwamba biashara yetu hii inategemea sana mafanikio ya jamii inayotuzunguka mafanikio ambayo tunaamini yataletwa na elimu," alisema.

Akizungumza kwenye hafla hiyo, Mkuu wa Wilaya ya Nzega, Naitapwaki Tukai pamoja na kuishukuru TCB alisema msaada huo umepatikana kwa wakati mwafaka kwa kuwa shule hiyo ipo kwenye mkakati wa kutafuta madawati zaidi kutokana na uhaba wa madawati unaoikabili shule hiyo.

Alisema shule hiyo inakabiliwa na uhaba wa madawati na kutoa wito kwa taasisi na mashirika mengine kuiga mfano wa benki hiyo kuisadia jamii.

# Maduka 21 ya UWT yateketea kwa moto

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

JUMLA ya maduka 21 kati ya 110 ya wafanyabiashara mtaa wa Kwivaha, mjini hapa mali ya jumuiya ya Wanawake wa Chama cha Mapinduzi (CCM UWT), Wilaya ya Njombe yameteketea kwa moto huku chanzo kikidaiwa kuwa ni hitilafu ya umeme.

Akizungumza na waandishi wa habari kwa niaba ya Kaimu Kamanda wa Jeshi la Zimamoto na uokoaji Mkoa wa Njombe, Mkaguzi Loth Madauda, alisema walipata taarifa ya moto huo Aprili mosi majira ya 3:28 usiku.

"Tulipata taarifa kwamba kuna tukio la moto mjini eneo la CCM baada ya hapo tukafika saa 3:31, tukakuta moto tayari umeshika kwenye fremu za maduka tukaanza kuzima moto na tumemaliza kuzima, " alisema Madauda.

"Jumla ya fremu za maduka zilizopo hapo ni 110, zilizoathirika ni 21 na zilizookolewa 89, kwa hiyo baada ya kumaliza kuzima moto sasa tunaendelea na uchunguzi kupata chanzo cha moto kwa sababu sasa hivi hatuwezi kusema, lakini inasadikiwa kuwa ni itilafu ya umeme baada ya moto kuwaka kuanzia kwenye nguzo ya umeme," alisema.

Katibu tawala Wilaya ya Njombe, Emmanuel George alisema chanzo cha awali cha moto huo ni hitilafu ya umeme huku uchunguzi wa ukiendelea kufanyika.

"Janga hili limekuwa sio la kwanza katika mji wetu nahisi mara ya tatu, nilikuwa nawaomba sana kwa kauli ya serikali tuzingatie sana taratibu za moto kwa maana ya wafanyabiashara, cha kwanza issue ya bima ya moto ni muhimu sana kwa wafanyabiashara, tuhakikishe tunapoondoka au kufunga maduka yetu hakuna umeme au kitu chochote kinachoweza kuanzisha moto usiwe umekiacha ndani," alisema George.

Katibu tawala aliwataka wafanyabiashara walioungulia maduka yao kuwa watulivu katika kipindi hiki kigumu wakati tathmini ikiendelea kufanyika ili kubaini hasara iliyotokea.

"Kauli ya serikali tunawapa pole sana baada ya tathimini kwa wale ambao wameunguliwa na bidhaa kwa maana ya kujua ni kiasi gani cha uhalibifu ambao umetokea, lakini kwa wale ambao tunajua biashara zetu unakuta wengi wanamikopo ya benki baada ya tathmini tutajua namna gani ya kukaa na mabenki kuwapa taarifa ili kuweza kuwapa auweni hawa watu waliokubwa na hili janga"alisema George.

Kwa upande wake katibu wa ccm mkoa wa Njombe Julius Peter, alilipongeza jeshi la zimamoto na uokoaji pamoja na wananchi kwa kujitokeza kuzima moto huo pamoja na kuokoa mali mbalimbali za wafanyabiashara huku akiwaomba wafanyabiashara kutulia wakati tathmini ya maafa itakapofanyika.

Polisi pia imewadhibiti vijana waliokuwa wakifanya uporaji wa mali kwenye maduka hayo.

# Uamuzi kesi ya kupotea mzee kutolewa Mei 10

**Na Tumaini Mafie,** ARUSHA

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Arusha, Mei 10 mwaka huu, inatarajia kutoa uamuzi wa kesi ya kulazimishwa kupotea kwa mkazi wa Kijiji cha Ololosokwani Wilaya ya Ngorongoro mkoani Arusha, Oriais Oleng'iyo (85).

Kesi hiyo namba 67 mwishoni mwa wiki ilikwenda mahakamani kwa ajili ya kusikilizwa mbele ya Jaji wa Mahakama hiyo, Mohammed Gwae.

Katika shauri hilo waleta maombi na wajibu maombi walipata nafasi ya kuwasilisha hoja zao mbele ya mahakama hiyo.

Upande wa waleta maombi walisema Mahakama ina mamlaka ya kuamuru mzee huyo kupelekwa mahakamani au kuachiwa huru aidha akiwa hai au amekufa.

Wakili wa utetezi katika kesi hiyo, Simoni Mbwambo alitoa madai ya kupigwa risasi na kupotezwa kwa Mzee Oriais Oleng'iyo ni matokeo ya operesheni iliyofanyika Loliondo Juni 10, mwaka jana wakati wa uwekaji vigingi eneo la vijiji 14 lenye ukubwa wa kilometa za mraba 1502.

Hata hivyo aliomba Mahakama iamuru walalamikiwa kumleta mahakamani Oriaisi Oleng'iyo ambaye amepelekwa kusikojulikana tangu alopokamatwa nyumbani kwake Engong'u Nairowa.

Aidha, Mbwambo alidai wamepeleka maombi hayo baada ya watu wengine waliokamatwa katika operesheni ya kuweka mipaka katika eneo la Pori Tengefu la Pololeti lililoko Ngorongoro kuachiwa na kesi yao kufutwa lakini mzee huyo hadi sasa hajulikani aliko.

Alidai walipopelekwa mahakamani Oriaisi hakuwa amejumuishwa na wenzake japokuwa shauri hilo liliondolewa mahakamani kwa kile kilichoelezwa kuwa Jamhuri haina nia ya kuendelea na shauri hilo.

"Baada ya washtakiwa kuachiwa huru Mzee Oriaisi hakuwa miongoni mwao, hivyo tukalazimika kukimbilia mahakamani kuomba kupatiwa mzee huyo kwa kuwa polisi ndiyo wanaojua aliko,"alidai Mbwambo.

Wkili mwingine wa waleta maombi, Joseph Oleshangay alidai kuwa wana amini mteja wao yupo mikononi mwa polisi kwa kuwa ndiyo waliomchukua siku ya vurugu zilipotokea.

Wakili wa wajibu maombi (Jamhuri),Peter Mseti alidai kwamba hakuna mahali waleta maombi waliposema au kutaja namba ya polisi au namba ya gari ya polisi zaidi ya kusema ni "difenda" ambapo inaweza kuwa gari yoyote.

Mseti alidai kuwa hawajawahi kumshikilia mtu huyo wala jina lake halijawahi kuonekana kwenye majina ya walioshikiliwa kuanzia Juni 8 hadi 20 kati ya wale waliokuwa na kesi.

# Watendaji kata sita za Longido wakabidhiwa pikipiki

**Na Allan Isack,** LONGIDO

WATENDAJI kutoka kata sita za Noondoto, Ilerienito, Gelai Lumbwa, Gelai Merugoi, Kamwanga na Elang'hatadapash wilayani Longido mkoani Arusha, wamekabidhiwa pikipiki kwa ajili kurahisisha utendaji kazi ikiwamo kutoa huduma kwa wananchi.

Akizungumza wakati akikabidhi pikipiki hizo, Mkurugenzi wa Mtandao wa Halmashauri ya Wilaya ya Longido, Stephen Ulaya, alisema pikipiki zimetolewa na serikali ili kuongeza ufanisi wa kutekeleza majukumu yao.

Hata hivyo, aliwataka watumishi hao kuzitumia pikipiki hizo vizuri na kwa umakini wa hali ya juu na kwa madhumuni ya kazi za serikali na siyo vinginevyo.

Kadhalika, aliwashukuru serikali kwa kutoa msaada wa pikipiki kwa watendaji wa kata hizo na aliahidi watazisimamia na kuzitunza kwa maslahi mapana ya wananchi wa halmashauri hiyo.

Mtendaji wa Kata ya Gelai, Merugoi Mollel, akizungumza kwa niaba ya watendaji wenzake, aliishukuru serikali kwa kutambua umuhimu wa kuwapatia pikipiki hizo, kwa kuwa zitawasadia hasa katika kuwahudumia wananchi wa kata zao.



Mhashamu Askofu wa Jimbo Katoliki la Moshi, Luvodick Minde akibariki matawi wakati wa ibada ya Jumapili ya matawi katika parokia ya Kristo Mfalme, mjini Moshi mkoani Kilimanjaro jana. **PICHA: MARY MOSHA**

# Wanafunzi 486 waingizwa kwenye madawati ya ulinzi, usalama

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

WANAFUNZI 486 wa shule za msingi na sekondari katika kata nne za Halmashauri ya Wilaya ya Babati mkoani Manyara, wameingizwa kwenye madawati ya ulinzi na usalama wa mtoto.

Lengo kuu ni kupaza sauti za kupinga ukatili wa kijinsia ambao unafanyika shuleni na majumbani na kuathiri maendeleo yao.

Taarifa za kuanzishwa kwa madawati hayo ilitolewa jana na Meneja Mkazi wa Shirika la So They Can (STC), Roselyne Mariki, wakati akizungumza na wadau wa elimu, walimu, viongozi wa wilaya, viongozi wa kata, dini na viongozi wa kimila.

Lengo lilikuwa ni kuwajengea uwezo juu ya namna ya kusimamia madawati hayo na kupinga ukatili wa watoto.

Mariki alisema wanafunzi wa shule za msingi ni 438 kutoka shule 28 na wanafunzi wa shule za sekondari ni 48 kutoka shule tano na kila shule inatoa wanadawati 16. Aidha, alisema wakati wanazungumza na wanafunzi waliwaeleza kuwa baadhi ya walimu wanawafanyia ukatili wa kingono, vipigo na matusi ambayo yanawaathiri kisaikolojia.


Vile vile alisema suala la ulinzi na usalama wa mtoto ndilo linawaongoza na ndiyo sababu wameamua kuanzisha madawati ya watoto katika shule wanazofanya nazo kazi.

Alisema baada ya kubaini madhaifu waliamua kutengeneza muongozo na kuufikisha kwa wadau mwaka huu ili wapange namna ya kutengeneza madawati hayo.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Babati, Anna Mbogo, alisema watahakikisha ukatili haufanyiki na kitu kitakachowasaidia ni kutoa chakula cha mchana shuleni kwa asilimia 96. Akizungumzia uundwaji wa madawati hayo, Mkuu wa Dawati la Jinsia kutoka Jeshi la Polisi mkoani Manyara, Mkaguzi Msaidizi wa Jeshi la Polisi, Wilness Kimario, alisema elimu hiyo itakuwa mkombozi na itapunguza vitendo vya ukatili.

Alisema asilimia 40 ya vitendo vya ukatili wanaofanyiwa watoto unafanyika shuleni.

Kimario alisema awali walidhani ukatili unafanyika kwa wanafunzi wa sekondari lakini pia unafanyika kwa wanafunzi wa darasa la awali na darasa la kwanza ambao wengi wao wana miaka minne mpaka sita.





# Bunge lapongeza uwekezaji uliofanywa na PSSSF

**Na Mwandishi Wetu,** MWANZA

KAMATI ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (PIC) imepongeza uwekezaji uliofanywa na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF) kwenye mradi wa kitega uchumi cha jengo la kibiashara jijini mwanza.

Wajumbe hao wakiongozwa na Mwenyekiti wake, Jerry Silaa walitoa pongezi hizo baada kutembelea mradi huo kwa lengo la kuona tija iliyopo kwenye uwekezaji.

Walisema uwekezaji wa jengo hilo umebadilisha sura ya Jiji la Mwanza, kwamba zamani eneo hilo lilitapakaa vibanda tu na kwamba uwekezaji umebadilisha sura ya Jiji la Mwanza jambo ambalo limeleta thamani ya kijamii.

Aidha wamesema uwekezaji wa mradi huo ni moja ya miradi iliyokamilika na yenye kutia matumaini hata, hivyo walishauri kufanywe marekebisho sehemu ambazo zina mapungufu ili kuvutia wapangaji kwenye maeneo ambayo bado hayana wapangaji. Aidha licha ya kupongeza uwekezaji huo pia walisema ripoti ya mradi iko vizuri na hasa kwa kamati inayoangalia uwekezaji wa mitaji ya umma na vipindi vya miradi kuanza kuingiza faida iliyokusudiwa.

Mwenyekiti wa PIC, Jerry Silaa licha ya kupongeza amebainisha kuwa pesa zilizowekezwa kwenye miradi ni pesa za wanachama na siyo za serikali, hivyo akashauri umakini ili kufikia malengo yaliyokusudiwa.

Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya PSSSF, Dk. Aggrey Mlimuka alisema bodi yake imepokea ushauri wa wajumbe na kuahidi kuyafanyia kazi maelekezo hayo ili kuongeza tija katika uwekezaji huo.

Mkurugenzi Mkuu wa PSSSF, Hosea Kashimba alisema jengo lina eneo la upangishaji lenye ukubwa wa mita 21,151.82 ambapo hadi Febrauri 2023 kampuni imepangisha jengo kwa kiwango cha asilimia 82.

Alisema maeneo ambayo tayari yamepangishwa kwa ujumla yana mita za mraba 17,436.07; kwa upande wa maeneo ambayo bado hayajapangishwa ni mita za mraba 3,715.75 ambayo ni sawa na asilimia 18.

# Ukosefu mitaji chanzo matumizi ya zebaki migodini

**Na Marco Maduhu,** MARA

WACHIMBAJI wadogo wa dhahabu katika mgodi wa Irasanilo uliopo Kijiji cha Magunga Halmashauri ya Wilaya ya Butiama mkoani Mara, wamesema licha ya zebaki kuwa na madhara katika uchenjuaji wamekuwa wakitumia kutokana na ukosefu wa mitaji.

Wamesema endapo serikali itaweka mpango mzuri wa kuwapatia mikopo kupitia taasisi za kifedha au mifuko ya serikali, wanaweza kupata mitaji na kununua vifaa vya kisasa kwa ajili ya kuchenjua dhahabu na kuondokana na matumizi ya kemikali ya zebaki.

Meneja wa mgodi huo, Robert Lucas, aliyasema hayo juni na kueleza kuwa wachimbaji tayari wameelimishwa na kufahamu madhara ya matumizi ya kemikali ya zebaki, lakini wanashindwa kuacha kuitumia kutokana na ukosefu wa mitaji ya kununua vifaa vya kisasa mbadala wa kemikali hiyo.

"Tunaziomba taasisi za kifedha zituamini sisi wachimbaji wadogo na kutukopesha pesa ili tupate mitaji na kununua vifaa vya kisasa vya kuchenjua dhahabu na kuondokana na matumizi ya kemikali ya zebaki ambayo ina madhara kiafya,"alisema Lucas.

Karani wa mgodi huo, Mugare Kitoki, alisema baada ya kuelimishwa juu ya madhara ya zebaki wameweka sheria inayokataza kufanya shughuli za uchenjuaji bila ya kuvaa vifaa kinga wala kuchoma dhahabu bila ya kuvaa viziba pua.

Pendo Kitone ni miongoni mwa wachenjuaji wa dhahabu alisema awali kabla ya kupewa elimu ya madhara ya zebaki walikuwa wakifanya kazi bila ya kuvaa vifaa kinga, lakini kwa sasa wanavaa vifaa hivyo.

Mmiliki wa mwalo wa kukamata dhadhabu ambao una kemikali ya zebaki, Wambura Mseti, alisema watumishi wake wakivaa 'groves' mikononi ukamataji wa dhahabu unakuwa mgumu. Alisema groves hizo wakati wa kusugua mchanga zinachanika na kusema ukwepaji wa madhara ya zebaki ni kutumia njia mbadala.

Kaimu Meneja wa Tathimini na Ufuatiliaji kutoka Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, Oswald Karadisi, akiwa mkoani Shinyanga Machi 7 mwaka huu, alisema katika baraza hilo kuna fursa mbalimbali za uwezeshaji.

Alisema kuna mifuko 73 ambayo inatoa ruzuku, mikopo ya moja kwa moja na dhamana na kuwataka wachimbaji wadogo wa madini wachangamkie fursa hiyo na kupata mitaji.




Ofisa Raslimali Watu Mwandamizi wa Barrick Bulyanhulu, Renatus Malawa, akizungumza na wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma juzi, wakati wa kongamano la kuwajengea uwezo wanafunzi wa vyuo vikuu, lililoandaliwa na taasisi ya AISEC Tanzania kwa udhamini wa kampuni ya Barrick. **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

# Plan International yawawezesha vijana 1,000 kujiajiri

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

VIJANA 1,000 kutoka kata 11 za Wilaya ya Ilemela na Nyamagana mkoani Mwanza wameanza kunufaika na mradi wa Sh. bilioni 4.7 wenye lengo la kuwawezesha katika shughuli za ujasiriamali. Mradi huo uitwao 'vijana maisha'unatekelezwa na Shirika la Plan International kwa vijana waliopo kwenye vikundi 58 kwa kufundishwa masuala ya ujasiriamali, utunzaji fedha, kilimo, ufundi.

Baada ya kuhitimu vijana hao hupewa vifaa vya kufanyia kazi kutokana na fani waliyochagua.

Akizungumza kwenye warsha ya kufunga mradi huo, Ofisa Mradi kutoka SEDIT, Nahum Fungo alisema mkopo wa Sh.milioni 66 ulitolewa kwa vikundi hivyo, huku vijana 600 wakifanya shuguli zao binafsi baada ya kupata ujuzi kutoka TAHA, VETA na SIDO.

Alisema kati ya vikundi hivyo viwili ni vya watu wenye ulemavu ambavyo vilipata zaidi ya Sh. milioni 21.

Mapolo Maneno kutoka SIDO alisema hatua ya Plan International kujenga jengo lenye mashine za usindikaji vyakula na uchakataji kemikali lililogharimu Sh. milioni 70 liliwanufaisha vijana wengi.

Mmoja wa wanufaika wa mradi huo, Victor Helman alisema kulingana na mafunzo waliyopewa ya usindikaji vyakula sasa wanamiliki mashine waliyoinunua kwa Sh.milion 1.5 inayowawezesha kusaga karanga na kufunga hadi mifuko 1,000.

Akifunga warsha hiyo, Ofisa Maendeleo ya Jamii Mkoa wa Mwanza, Janeth Shishila, aliwataka vijana hao kutumia mitandao ya kijamii kutangaza bidhaa zao, kutunza mashine walizopewa na kuzitumia kwa malengo husika.

Pia aliwaagiza maofisa maendeleo ya jamii pamoja na watendaji wa kata kufuatilia mashine hizo ili vijana hao wasiziuze au kufanyia matumizi ambayo hayajakusudiwa.

Meneja wa Shirika la Plan International, Majani Rwahambali aliwaomba viongozi wa serikali katika ngazi za kata na vijiji kuwasimamia vijana hao kutumia vifaa walivyopewa kwa malengo yaliyokusudiwa.

Nipashe
Spotika



ARSENAL WANAWEZA KUSHINDA UBINGWA WA EPL MSIMU HUU? UK. 12-13



OSIMHEN

# MASTRAIKA WA5 WANAOWEZA KUSAJILIWA MANCHESTER UTD

## ISIKUPITE

KATIKA hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika iliyomalizika Jumamosi iliyopita. Raja Casablanca kutoka Kundi C ndiyo timu iliyomaliza na pointi nyingi zaidi 16, ikifuatiwa na Mamelodi Sundowns (14) kutoka Kundi B, kisha Wydad Casablanca (13) Kundi A na Esperance Sportive de Tunis, iliyomaliza kileleni kwenye Kundi D ikiwa na alama 11. Timu zingine zilizofuzu kwa kumaliza nafasi ya pili na alama zao ni Al Ahly (10), JS Kabylie (10), CR Belouizdad (10) na Simba (9).

**MANCHESTER,** England

KLABU ya Manchester United inakaribia kuingia katika dirisha la usajili la majira ya joto kusaka mshambuliaji mahiri. Baada ya kuondoka kwa Cristiano Ronaldo Novemba, United ilimnunua Wout Weghorst kwa mkopo katika dirisha la uhamisho la Januari.

Kiwango cha juu cha kazi cha Weghorst na sifa za kiufundi zimewasaidia 'Mashetani Wekundu' hao. Hata hivyo, ustadi wake wa kupachika mabao haujaboreshwa kama vile Manchester United wangependa. Kwa hiyo, klabu itatafuta kusajili mshambuliaji mahiri ambaye anaweza kufunga mabao kila msimu.

Washambuliaji kadhaa wa juu tayari wamehusishwa na Mashetani Wekundu. Kocha Erik ten Hag anastahili kuungwa mkono katika dirisha la usajili la majira ya joto na kusajili mshambuliaji mahiri kunaweza kumsaidia kuifanya timu hii kuwa bora zaidi.

Hebu tuwaangalie washambuliaji watano mahiri ambao Man United wanaweza kusajili msimu huu wa joto...

### #5 Randal Kolo Muani (Eintracht Frankfurt)

Randal Kolo Muani amekuwa kiongozi wa Eintracht Frankfurt msimu huu. Amefunga mabao 16 na kutoa pasi za mabao 14 katika mechi 35 alizocheza kwenye michuano yote akiwa na kikosi hicho cha Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, hadi sasa msimu huu.

Hajaishia hapo na kwa sasa yupo kwenye nafasi ya kugombea namba tisa kwenye kikosi cha kwanza cha Ufaransa. Kwa mujibu wa L'Equipe (kupitia The Metro), Kolo Muani yuko juu kwenye orodha ya matamanio ya Ten Hag msimu huu wa majira ya joto.

Manchester United wameripotiwa kuwa tayari kutoa kitita cha euro milioni 120 kwa mshambuliaji huyo mwenye umri wa miaka 24. Anaweza kuwa nyongeza kwa kikosi cha vijana na cha kusisimua cha Mashetani Wekundu hao.

### #4 Marcus Thuram (Borussia Monchengladbach)

Mshambuliaji wa Borussia Monchengladbach, Marcus Thuram, anatarajiwa kuondoka kwenye klabu hiyo ya Bundesliga kama mchezaji huru mkataba wake utakapomalizika msimu huu wa majira ya joto. Gladbach hakuweza kumfunga mshambuliaji huyo wa kati kwa mkataba mpya na amekuwa akihusishwa na klabu kadhaa za Ligi Kuu England.

Man United itakabiliana na ushindani mkali kutoka kwa Newcastle United huku Magpies hao wakiwa na nguvu ya kifedha ya kumpa dili nono mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25. Thuram ndiye chaguo bora zaidi la bajeti ambalo Manchester United wanalo mbele yao.

Mfaransa huyo amefunga mabao 15 na kutoa pasi nne za mabao katika mechi 26 alizocheza kwenye michuano yote akiwa na Borussia Monchengladbach hadi sasa msimu huu.

### #3 Goncalo Ramos (Benfica)

Goncalo Ramos alijitangaza kwenye Kombe la Dunia la FIFA 2022 kwa kufunga hat-trick katika mchezo wake wa kwanza wa mashindano hayo kwa Ureno dhidi ya Uswisi. Ameonesha uwezo wake wa kushambulia na amekuwa katika kiwango cha kuvutia Benfica msimu huu.

Kinda huyo wa Ureno amefunga mabao 24, na kutoa pasi 10 za mabao kwenyemechi 36 katika michuano yote akiwa na wababe hao wa Ureno hadi sasa. Ramos ana umri wa miaka 21 pekee na anaweza kuwa suluhisho la muda mrefu kwa tatizo la mshambuliaji pale Man United. Lakini amefungwa na Benfica hadi mwaka 2026 na klabu hiyo ya Ureno inajulikana kwa kupenda bei kubwa kuwauza nyota wao wachanga.

### #2 Harry Kane (Tottenham Hotspur)

Harry Kane ni mmoja wa washambuliaji bora wa kizazi chake. Lakini ikiwa atasalia Tottenham Hotspur, kuna nafasi kwamba historia yake inaweza kufafanuliwa kwa kuwa na fedha nyingi tofauti na mafanikio yake binafsi.

Kwenye karatasi, Kane na United wanaonekana kama mechi bora. Kane ana nguvu kubwa kwenye Ligi Kuu England na atakuwa nyongeza nzuri kwa Man United. Mkataba wa sasa wa Kane na Spurs unamalizika 2024 na huenda lisiwe wazo baya zaidi kwao kumnunua msimu huu wa majira ya joto.

Kane ana umri wa miaka 29, na ana uwezekano wa kukaa kileleni mwa mchezo wake kwa angalau misimu mitatu au minne zaidi. Lakini Mwenyekiti wa Tottenham, Daniel Levy, hatairuhusu Man United kumpata kirahisi.

### #1 Victor Osimhen (Napoli)

Victor Osimhen amekuwa mmoja wa nyota bora wa msimu wa 2022-23 barani Ulaya. Amekuwa mfungaji wa kutegemewa ambaye ana uwezo wa kuwatesa mabeki mara kwa mara. Kiwango cha mshambuliaji huyo wa Nigeria kimekuwa muhimu sana kwa Napoli kutwaa ubingwa msimu huu.


Osimhen amefunga mabao 25 na kutoa pasi tano za mabao katika mechi 29 alizocheza kwenye mashindano yote akiwa na Napoli hadi sasa msimu huu. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24, anahusishwa na Man United na wababe hao wa Serie A watafanya vema kumbakisha katika klabu hiyo zaidi ya msimu huu wa majira ya joto.

NIPASHE JUMATATU APRILI 3, 2023



## Extra Time

# ARSENAL WANAWEZA KUSHINDA UBINGWA EPL MSIMU HUU?



Gabriel Jesus, katika harakati za kuifungia Arsenal kwenye mechi dhidi ya Leeds United, iliyopigwa Uwanja wa Emirates juzi, Jumamosi na Gunners kushinda 4-1. **PICHA: MTANDAO**

**LONDON,** England

KUITAZAMA timu hii ya Arsenal ikicheza msimu huu kumewapa mashabiki wengi matumaini kwamba 'Washikabunduki' hao huenda wakamaliza ukame wao wa ubingwa wa Ligi Kuu. Mara ya mwisho waliponyanyua taji la Ligi Kuu ya England ilikuwa mwaka wa 2004, huku wakimaliza ligi bila kupoteza.

**Kama misimu mingi ya hivi karibuni, Manchester City ilitarajiwa kuibuka na ushindi mwingine wa taji, haswa kwa kumnunua mshambuliaji wa Norway, Erling Haaland, anayeongoza katika mbio za kuwania Kiatu cha Dhahabu cha Ligi Kuu akiwa amefunga mabao 28 hadi sasa.**

Lakini Arsenal wanaonekana kama wanaweza kuzuia matarajio yao na kwa sasa wapo nafasi ya kwanza kwa pointi nane huku City wakiwa na mchezo mkononi. Hapa chini, tunajaribu kuangalia kama wababe hao wa London Kaskazini wanaweza kufikia jambo lisilofikirika.

### #Takwimu

Kutazama msimu huu ukikamilika, wengi hawangefikiria Washikabunduki hao kuwa katika nafasi waliyomo kwa sasa. Kwa kutumia takwimu za FBREF za msimu wa Ligi Kuu ya 2022-23 hadi sasa, tunaweza kujaribu kuhitimisha kwa nini wanafanya vema.

Washikaji hao wa London Kaskazini wamecheza jumla ya michezo 28 hadi sasa msimu huu, wakishinda mara 23, sare tatu na kupoteza tatu. Wamefunga wastani wa mabao 2.46 kwa kila mchezo na katika safu ya ulinzi wamekuwa wakifanya vema sana, wakiruhusu mabao 0.93 kwa kila mchezo, kwa mujibu wa FBREF (kabla ya mechi za mwishoni mwa wiki) ambapo wallishinda 4-1 dhidi ya Leeds United.

Arsenal wamefunga jumla ya mabao 66 (ukiacha manne dhidi ya Leeds mwishoni mwa wiki), ambapo wamevuka matarajio ya kufunga kwa msimu mzima. Kulingana na xG yao (malengo yanayotarajiwa), walitarajiwa tu kufunga jumla ya mabao 53.8. Hata hivyo, wamefunga mabao 13 zaidi ya walivyotarajiwa kufunga, ambayo ni moja ya chanya tunaweza kuiangalia msimu huu.

Takwimu nyingine ambayo Arsenal wanayo kwa sasa ni mabao yanayotarajiwa dhidi ya xGA. Wameruhusu mabao 26 (kabla ya lile moja dhidi ya Leeds) mwishoni mwa wiki, hadi sasa msimu huu, na xGA ya FBREF inatarajia kufungwa mabao 27 hadi sasa msimu huu. Hawafanyi vizuri sana, lakini wanafanya vizuri zaidi kuliko inavyotarajiwa.

### #Wafungaji Mabao wa Arsenal

Moja ya sababu zinazotia matumaini kwa nini Arsenal wanaweza kushinda ligi kweli ni kwamba mabao yanatoka kila upande uwanjani. Kuanzia safu ya ulinzi hadi kiungo hadi mbele. Wamekuwa na jumla ya wafungaji 18 tofauti hadi sasa msimu huu.

Gabriel Martinelli na Bukayo Saka wamefunga mabao mengi zaidi hadi sasa wakiwa na mabao 13 kila mmoja, huku Martin Odegaard akiwa amefunga mabao 10, akichangia jumla ya mabao 36. Pia wamechangia jumla ya pasi 20 za mabao kati yao katika mashindano yote.

Saka amekuwa mmoja wa cheche zinazong'ara zaidi kwa klabu hiyo msimu huu, akitengeneza nafasi kwenye safu hiyo ya kulia, pamoja na kufunga na kusaidia mabao. Kwa sasa anajivunia mabao 13 na asisti 10, uwiano mkubwa wa mabao na pasi za mabao kikosini.

Arsenal wamecheza soka la wazi na wamefunga mabao mazuri msimu huu, ambayo yatakumbukwa kwa miaka mingi.

### #Mikel Arteta

Mikel Arteta, katika msimu wake wa tatu kamili akiinoa Arsenal ameona mambo mengi mazuri na maboresho katika muda wake wote hapa. Ameonesha uwezo wa kutumia wachezaji tofauti katika nafasi tofauti. Ununuzi wake katika madirisha kadhaa ya uhamisho umewafanya wababe hao wa London kuwa timu yenye nguvu zaidi.

Kupatikana kwa Gabriel Jesus na Oleksandr Zinchenko kumeisukuma timu hiyo kufikia kiwango kipya kabisa. Zinchenko amekuwa mbadala wa Kieran Tiereny, ambaye amekuwa na matatizo ya majeraha katika msimu mzima uliopita.

Mikel Arteta amemsajili Zinchenko kama nafasi ya beki wa pembeni, akitoa msaada kwa safu ya kati huku Jesus akicheza kama tisa ya uongo, au anatoka kuelekea kwenye mbawa. Saka na Martinelli mara nyingi wamepata nafasi ya kufanya kazi kati zaidi na wamekuwa hatari sana, wakifunga mabao kwa kufurahisha.

Arteta amekuwa akisimamia kikosi vema kwa kupokezana na mbinu dhidi ya wapinzani ambao Arsenal wanakabiliana nao msimu huu wote. Mhispania huyo amekuwa miongoni mwa sababu kwa Washikabunduki hao kuzidisha matarajio ya msimu huu.

Arsenal wanauwezekano na kuzidi matarajio msimu huu. Ikiwa watashinda Ligi Kuu, ushindi huu utakumbukwa kwa miaka.

## Nukuu

"Yeye ni mchezaji wangu bora wa msimu kwa wakati huu. Anazidi kuwa bora na bora na amekuwa mwiba kwa watu wa Ukraine. Yeye ni mmoja wa majina ya kwanza kwenye karatasi hii ya timu, hata huna haja ya kuangalia zaidi," **Beki wa zamani wa England, Stuart Pearce, akiamini nyota wa Arsenal, Bukayo Saka, anastahili kuwa mchezaji bora wa msimu, wakati akionyesha kiwango bora kwenye mechi ya kimataifa dhidi ya Ukraine.**



"Dini ni muhimu sana kwangu. Ninaheshimu sheria za Kiislamu na ninasali mara tano kwa siku, kila mara. Sigusi pombe. Hakukuwa na mgongano kati ya dini na ukweli kwamba nilitaka kucheza mpira wa miguu. Nililelewa kwa usahihi na kwa njia sahihi na wazazi wangu wanajivunia ukweli kwamba mimi ni mwanasoka," **Mshambuliaji wa Senegal na Bayern Munich, Sadio Mane akizungumzia umuhimu wa Uislamu katika maisha yake.**



"Nimetimiza kwa hili; ni kile nilichokuwa nakikosa. Namshukuru Mungu nimepata kila kitu kwenye soka. Vikombe hivi huwa naviweka kwenye jumba la makumbusho nyumbani. Asante kwa CONMEBOL kwa kutuenzi na kwa wimbo pekee, tunasikiliza sana na inanikumbusha wakati anaimbiwa Diego [Maradona].Tunaishi nyakati nzuri sana, tulikuwa na bahati kurudi Argentina baada ya Kombe la Dunia na tulipokea maneno mengi ya mapenzi. Ilikuwa tofauti, ndivyo watu wa Argentina walionyesha," **Lionel Messi baada ya wiki iliyopita kutunukiwa tuzo ya heshima ya sanamu yake kuwekwa makao makuu ya Chama cha Soka cha Amerika Kusini (CONMEBOL) pembeni ya manguli wa soka, nyota wa Brazil, Pele na Muargentina mwenzake, Diego Maradona.**





KUITAZAMA timu hii ya Arsenal ikicheza msimu huu kumewapa mashabiki wengi matumaini kwamba 'Washikabunduki' hao huenda wakamaliza ukame wao wa ubingwa wa Ligi Kuu. Mara ya mwisho waliponyanyua taji la Ligi Kuu ya England ilikuwa mwaka wa 2004, huku wakimaliza ligi bila kupoteza.

Uk. 12&13



Simon Msuva (aliyefunga bandeji mkononi), akifurahia kwa kupiga 'selfie' na wachezaji wenzake wa Taifa Stars baada ya kuifungia timu yake bao pekee wakati wakishinda 1-0 ugenini nchini Misri dhidi ya Uganda Cranes kwenye mechi ya kuwania kufuzu Afcon 2023 kabla ya kukutana na kipigo kama hicho mchezo wa marudiano Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam siku nne baadaye. **PICHA: MTANDAO**

# STARS NA REKODI MBAYA NYUMBANI, NZURI UGENINI

**Na Adam Fungamwango**

HAKUNA Mtanzania aliyeamini kuwa Timu ya Taifa ya Tanzania, Taifa Stars, imepoteza mechi yake mara baada ya mwamuzi Ahmad Heeralall, kutoka Mauritius kupuliza kipenga kuashiria kumalizika mechi ya kusaka tiketi ya kufuzu Fainali za Mataifa ya Afrika (Afcon) 2023, na Tanzania ikiwa imepoteza kwa bao 1-0 dhidi ya Uganda Cranes.

**Hadi dakika za mwisho kabisa hakukuonekana dalili yoyote ya Stars kupoteza mechi hiyo. Ilikuwa ndiyo inashambulia, huku ambao hawakuamini kama bao litafungwa basi walijua itakuwa suluhu.**

Ghafla tu shambulizi la kushtukiza lililotengenezwa na wachezaji wawili, ambalo lilionekana halina madhara yoyote, ndilo lililoiua Stars, likizima ndoto ya kufuzu mapema zaidi fainali hizo zitakazochezwa nchini Ivory Coast Januari hadi Februari mwakani.

Ikiwa kwenye Kundi F, Tanzania bado inaendelea kushika nafasi ya pili, lakini ni kwa alfabeti tu dhidi ya Timu ya Taifa ya Uganda ambayo ipo nafasi ya tatu, zote mbili zikiwa na pointi nne, zimeshinda mechi moja, sare moja, kupoteza mbili, zikifunga mabao manne kila moja.

Stars sasa inatakiwa ifanye vema kwenye mechi zake zote mbili zilizobaki dhidi ya Niger nyumbani na Algeria ugenini na kuiombea mabaya Uganda ili iweze kufuzu kwa mara ya tatu fainali za Afcon.

Baada ya mechi hiyo, kila shabiki aliongea lake kwa sababu wengi walidhani huenda Stars ingeweza kushinda kwa idadi kubwa ya mabao kwa sababu tu siku nne zilizopita kabla ya hapo ilishinda bao 1-0 nchini Misri.

Kitu ambacho wengi wamesahau ni kwamba Taifa Stars ina rekodi ya kushangaza ya kuweza kushinda au kutoa sare ugenini, lakini katika hali ilisiyotarajiwa inapoteza nyumbani. Katika makala haya tunazidondosha rekodi hizo, twende sasa...

**#Msumbiji 0-0 Taifa Stars (2006)**

Mwaka 2006, Tanzania ilianza kampeni yake kabambe ya kuhakikisha inacheza Fainali za Mataifa ya Afrika (Afcon) zilizochezwa 2008 nchini Ghana. Kulikuwa na hamasa na kaulimbiu nyingi kuwa ni lazima Stars icheze fainali hizo.

Na kweli ilianza kuonekana hivyo baada ya mechi ya kwanza kwenda kutoka suluhu ugenini dhidi ya wenyeji Msumbiji, mechi ya Kundi G iliyochezwa Oktoba 8, 2006

**#Burkina Faso 0-1 Taifa Stars (2007)**

Moja kati ya matokeo ya kushangaza kabisa na ya kufurahisha yaliyotokea mwaka 2007, yalikuwa kwa mara ya kwanza Tanzania kwenda kuifunga timu ya Afrika Magharibi nchini kwao.

Ilikuwa ni harakati za kuisaka tiketi ya kwenda kucheza Fainali za Mataifa ya Afrika nchini Ghana mwaka 2008. Stars ikiwa kwenye Kundi G, iliichapa Timu ya Taifa ya Burkina Faso bao 1-0 ikiwa ugenini. Bao pekee kwenye mechi hiyo iliyochezwa Juni 16, lilifungwa na Erasto Nyoni wakati huo akichezea Vital'O ya Burundi.

Kwenye mechi ya kwanza ya kundi ambayo ilichezwa nchini Septemba 2, mwaka 2006, Stars ilishinda nyumbani mabao 2-1.

**#Taifa Stars 0-1 Msumbiji (2007)**

Ulikuwa ni usiku wa balaa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, wakati huo ukiitwa wa Taifa, baada ya dakika 90 kumalizika ubao ukisomeka Stars 0-1 Msumbiji.

Baadhi walilia machozi na kutoamini kilichotokea kwa sababu Tanzania ilihitaji ushindi ili ifuzu hatua ya fainali na ilionekana ingekuwa hivyo.

Kwa sababu Oktoba 8, 2006, Stars ilitoka suluhu dhidi ya ya Msumbiji jijini Maputo, hivyo ilionekana ushindi ungekuwa si kazi ngumu sana ukilinganisha na hamasa zilizowekwa.

Ilikuwa ni Septemba 8, 2007, wakati ndoto za Watanzania kwenda Afcon 2008 nchini Ghana zilipokatishwa na straika hatari wakati huo, Tico Tico. Senegal ndiyo iliyofuzu kwenye kundi hili. Hii ndiyo imekuwa ni mbaya na ya majonzi zaidi kwa Stars kupoteza nyumbani.

**#Taifa Stars 0-1 Benin (2021)**

Ikiwa kwenye Kundi J, Stars ilianza safari ya kusaka tiketi ya kwenda nchini Qatar kucheza fainali ya Kombe la Dunia lililochezwa mwaka jana. Moja ya timu iliyokuwa kwenye kundi hilo ni Benin. Kama kawaida, Stars ilipoteza mechi yake kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa ikichapwa bao 1-0 Oktoba 7, 2021.

**#Benin 0-1 Taifa Stars**

Siku tatu baadaye, Oktoba 10 nchini Benin, Stars iliendeleza rekodi yake ya kushangaza, baada ya kwenda kushinda ugenini bao 1-0 dhidi ya timu ambayo iliishindwa ikiwa nyumbani.

**#DR Congo 0-0 Taifa Stars**

Kwenye michuano hiyo hiyo ya kusaka tiketi ya kucheza Kombe la Dunia, Stars ilikwenda nchini Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo na kuilazimisha sare timu ya taifa ya nchini hiyo, zikifungana bao 1-1, mchezo ukipigwa Septemba 2, 2021.

**#Taifa Stars 0-3 DR Congo**

Wakati kila Mtanzania akidhani kwa sababu Wakongomani walilazimishwa sare kwao, basi hawatoki kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, rekodi ikajirudia, Stars ikakung'utwa mabao 3-0, Novemba 11, 2021, na kuzima ndoto za Watanzania kukata tiketi ya kwenda Qatar.

**JE, WAJUA?**



HII ni mara ya kwanza kwa Bukayo Saka, kuanzia benchi katika mechi za Ligi Kuu England akiwa na Arsenal baada ya kuanza mechi 54 mfululizo. Katika mechi dhidi Leeds wakati wakishinda 4-1 juzi, Jumamosi, Mikel Arteta alimuanzishia benchi winga huyo.



# Mpango kuzindua mchakato Dira ya Taifa ya Maendeleo leo

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MAKAMU wa Rais Dk. Philip Mpango, leo anatarajiwa kuzindua mchakato wa maandalizi ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 ambayo itatoa maono na kuweka malengo ambayo taifa linataka kuyafikia ndani ya kipindi cha miaka 25 ijayo.

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango, Jenifer Omolo, alibainisha hayo juzi alipokuwa akitoa taarifa kuhusu uzinduzi wa mchakato huo kwa waandishi wa habari jijini hapo.

"Dira hii itatoa maono na kuweka malengo ambayo taifa letu linataka kuyafikia ndani ya kipindi cha miaka 25 ijayo baada ya kuisha kwa kipindi cha utekelezaji wa dira tuliyo nayo sasa ya Taifa ya Maendeleo 2025.

"Maandalizi ya dira mpya ya mwaka 2050 yanakidhi matakwa ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo ndiyo mwongozo mkuu wa nchi yetu,"alisema Omolo.

Aidha, alisema mnamo mwaka 2009/10, serikali ilifanya tathmini ya utekelezaji wa Dira ya mwaka 2025 kupitia mikakati na programu za maendeleo.

Alisema tathmini hiyo ilibainisha uhitaji wa taifa kuanza kupanga vibaumbele vya nchi.

Vile vile, alisema mpango huo wa miaka 15 ulipangwa kutekelezwa kwa mipango ya muda wa kati ya miaka mitano na mipango ya muda mfupi ya mwaka mmoja.

Kadhalika, alisema ili kufanikisha maandalizi ya Dira ya Taifa ya Maendeleo yam waka 2050 inategemea ushiriki wa wadau wote.

# Majaji, mahakimu wanolewa kuhusu haki za binadamu

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MTANDAO wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC) umetoa mafunzo ya siku mbili kwa mahakimu na majaji kuhusu wajibu wa Mahakama katika kutunza na kulinda uhuru wa kujieleza pamoja na haki za binadamu.

Mratibu wa THRDC, Onesmo Olengurumwa akizungumza na waandishi wa habari juzi jijini hapa wakati wa ufunguzi wa mafunzo hayo alisema lengo ni kukumbushana wajibu katika kutekeleza majukumu ya kila siku.

"Lengo la mafunzo haya ni kukumbushana masuala mbalimbali katika utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku kwa sababu kumekuwepo na mabadiliko mengi ya kisheria na masuala mbalimbali yanayohusu haki za binadamu, hivyo wao kama watu ambao wanatoa haki kila siku katika Mahakama, wanapaswa kuyafahamu ili kulinda haki za binadamu na uhuru wa kujieleza,"alisema Olengurumwa.

Alisema pia mafunzo mengine ambayo yatatolewa ni masuala ya maadili kwa mahakimu na majaji katika utekelezaji wa majukumu ya utoaji wa haki katika maeneo yao.

"Suala la maadili ni jambo la muhimu sana katika Mahakama zetu nchini, hivyo mafunzo haya pia yatasaidia kuwakumbusha mahakimu na majaji wajibu wao wa kutenda haki kwa kuzingatia maadili ya kazi zao,"alisema Olengurumwa.

Alisema utoaji wa mafunzo hayo ni sehemu ya mtandao huo kuunga juhudi za serikali katika kuboresha miundombinu ya utoaji haki nchini.

"Tusiwe watu wa kulalamika tunapaswa kushiriki kuboresha Mahakama zetu kufanya kwa pamoja kama taifa. Huduma ya Mahakama ni huduma ya haki, jukumu letu kusaidia kuboresha sekta hii ili kupunguza malalamiko yaliyopo kwa wananchi katika masuala ya haki jinai,"alisema Olengurumwa.

Naibu Katibu Mkuu wa Chama cha Mahakimu na Majaji Tanzania (JMAT), Mary Kallomo, alisema mafunzo hayo yatawasaidia kuboresha utendaji wao wa kila siku katika kulinda haki za binadamu na uhuru wa kujieleza.

"Tunahitaji kukumbushana masuala mbalimbali katika utekelezaji wa majukumu yetu na suala la maadili ni jambo la muhimu sana kwakuwa sisi ndiyo tunatoa haki katika Mahakama zetu,"alisema

Hata hivyo, alisema ipo haja kwa wadau wa masuala ya haki jinai nchini kutoa mafunzo kwa kundi hilo kuhusu masuala ya kimtandao.



Ofisa Mtendaji wa Kata ya Chamwino, jijini Dodoma, Lucas Venance akizungumza na wakazi wa kata hiyo jana, alipokuwa akiwahimiza kufanya usafi wa mazingira kwenye maeno yao. Katikati (waliosimama) ni Msimamizi usafi wa mazingira wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma, John Lugendo. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Bunge lawataka wananchi kutumia fursa za REA

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

KAMATI ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (PIC), imewataka wananchi kutumia fursa ya umeme unaosambazwa na Wakala wa Nishati Vijijini (REA) kwa kubuni shughuli za biashara zinazotumia nishati hiyo.

Ilitoa rai hiyo juzi baada ya kutembelea Shule ya Sekondari ya Irisya iliyopo wilayani Ikungi mkoani hapa, kukagua umeme wa REA uliofikishwa shuleni hapo na katika vijiji vitatu vya Kata ya Irisya.

"Umeme ni fursa, hivyo wananchi kwa kuwa umeme umeshawafikia mnaweza kufanya shughuli za kiuchumi na za uzalishaji na kwa kufanya hivyo mtachochea shughuli za kiuchumi katika Kata ya Irisya," alisema Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Vuma Augustino.

Augustino alisema kwa kuwa zaidi ya Sh.bilioni 50 zimetengwa kwa ajili ya kupeleka umeme katika vijiji vyote vya Mkoa wa Singida na wakandarasi tayari hivyo REA ihakikishe inawasimamia wakandarasi hao kwa ukaribu ili waweze kumaliza kazi hizo ndani ya mkataba.

Mwenyekiti wa Bodi ya Nishati Vijijini (REB), Janet Mbene, alisema la REA ni kuhakikisha kila kijiji kinapata umeme ambao utawasaidia wananchi kiuchumi, kijamii na kimaendeleo.

"Wanafunzi wa Shule ya Sekondari Irisya tumewaona wakifanya kwa vitendo kwenye maabara ya sayansi na hii imeongeza elimu kwao na hii sisi kwetu ni furaha na tumetimiza malengo yetu tuliojiwekea," alisema.

Mbene alisema wananchi watumie fursa hii kwa kuunganisha umeme katika maeneo yao ya makazi na biashara na kubuni biashara ambazo zinatumia umeme kujinufaisha kuleta maendeleo ya mmoja mmoja na ya jamii kwa ujumla.

Mwenyekiti huyo aliongeza miradi mingi ya REA tayari ina fedha ya kuitekeleza kwa hiyo jukumu la REA ni kuhakikisha wakandarasi ambao wamepewa kazi kuweka umeme wanaifanya kikamilifu na kwa ubora unaotakiwa.

Meneja wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) Mkoa wa Singida, Mhandisi Florence Mwakasege, alisema shirika hilo linafanya kazi kwa ushirikiano kwani ilipo REA na TANESCO ipo.

Kwa mujibu wa maelekezo ya Waziri wa Nishati, January Makamba, ni kwamba hadi ifikapo Desemba 2024 vijiji vyote ambavyo havina umeme vitakuwa vimefikiwa na huduma hiyo nchi nzima.





# Watumishi watakiwa kujiunga vyama vya wafanyakazi

Na Grace Mwakalinga,
MBEYA

WATUMISHI wapya wa umma wanaoajiriwa Wilaya ya Rungwe mkoani Mbeya, wametakiwa kujiunga na vyama vya wafanyakazi vinavyotetea haki na maslahi yao kwa mujibu wa sheria za nchi, badala ya kuingia kwenye vyama vyenye mrengo wa harakati hasi za kupambana na serikali kwa madai kuwa vitawasababishia migogoro na waajiri wao.

Rai hiyo imetolewa na Mkuu wa Wilaya ya Rungwe, Jaffari Haniu, kupitia hotuba yake ambayo ilisomwa mwishoni mwa wiki na Ofisa Tawala wa eilaya hiyo, Amimu Mwandelile, kwenye hafla ya kuzindua gari jipya la Chama cha Walimu (CWT) wilayani humo. Alisema ni muhimu watumishi kabla ya kujiunga na vyama hivyo wakafanya utafiti kujua shughuli wanazozifanya ili kuepuka kuingia kwenye makundi ambayo yamekusudia kuichafua serikali, aliwataka kuwa wazalendo kwa nchi yao.

"Kuna vyama vingine vinaanzishwa kwa lengo la kuichafua serikali au kuikosea kwa kila jambo linalofanyika sasa hatutamani na nyie hapa Rungwe yatokee haya fanyeni kazi kwa bidii watumishi wapya jiungeni kwenye vyama ili kutetea maslahi yenu kwa njia zinazofaa," alisema Mwandelile.

Mwenyekiti wa CWT, Wilaya ya Rungwe, Mathew Chawala, alisema uwepo wa amani kwenye vituo vya kazi, utaongeza ufaulu wa wanafunzi.

Alisema CWT wamekuwa kielelezo cha kuhubiri amani na utulivu kwa taifa kupitia shughuli wanazozifanya mbali na ufundishaji wa watoto, huanzisha miradi mbalimbali kwa ajili ya kuinuana kiuchumi na kusaidiana kwenye shida na raha.

Katibu wa CWT Shoide Charles alisema Sh milioni 67 zimetumika kununua gari hilo aina ya Coaster mayai ambalo litatumika kwa ajili ya shughuli mbalimbali za kujiingizia kipato na kwenye shida na raha baina yao.

Mwalimu wa Shule ya Msingi Kisa, Philbert Mkuto, alipongeza uongozi wa CWT kwa kuzitumia zilizovyokusudiwa fedha zilizotolewa na kwamba gari hilo litasaidia kuboresha shughuli zao na kukabiliana na shughuli za kijamii.




Mkuu wa Shule ya Msingi Kunduchi, Moses Amani (wa tatu kushoto), akiwa na Rais wa Klabu ya Rotary ya Dar es Salaam, Nikki Aggarwal (wanne kushoto) pamoja na baadhi ya wanafunzi na waalimu wa shule hiyo, baada ya kupokea msaada wa madawati 300 yenye thamani ya Sh. milioni 38 kutoka kwa klabu hiyo, mwishoni mwa wiki. Klabu hiyo, imeshatoa zaidi ya madawati 2,300 yenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 300 kwa shule mbalimbali za msingi za mkoa wa Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

# Wazalishaji wadogo wapewa fursa kusajili bidhaa bure

Na Grace Mwakalinga,
MBEYA

WAZALISHAJI wadogo wa mafuta ya kupikia mkoani Mbeya ambao wamekidhi vigezo vya ubora, wametakiwa kujitokeza kusajili bure bidhaa zao na kupata nembo ya ubora ya Shirika la Viwango nchini (TBS) ili bidhaa zao ziweze kukubalika katika soko la ndani na nje ya nchi.

Maofisa kutoka Shirika la Viwango nchini TBS hivi karibuni wakiwa jijini Mbeya waliwatembelea wajasiriamali kwa lengo la kutoa elimu na kuwakumbusha umuhimu wa kusajili biashara zao.

Ofisa Masoko wa Shirika hilo, Debora Haule, alisema waliwafikia wajasiriamali wa Wilaya ya Chunya, Rungwe, Busokelo, Kyela na Halmashauri ya Jiji la Mbeya na maeneo wanapofanyia shughuli zao katika masoko, magulio kutoa elimu ya udhibiti ubora wa bidhaa wanazozalisha na kuziuza.

Alisema zaidi ya wajasiriamali 10,000 wa Mkoa wa Mbeya walipatiwa elimu ya matumizi ya nembo zilizothibitishwa ubora wa bidhaa wanazozalisha na TBS kwa gharama bure za usajili wa bidhaa zao.

"Serikali imeamua kulipa gharama zote za usajili wa bidhaa za wajasiriamali ambazo zinahitaji nembo ya udhibiti ubora jukumu letu TBS ni kuwaeleza haya ili kutumia fursa hiyo kuthibitishiwa ubora na kupata nembo ambayo itawapa uhakika wa kuuza vitu vyao ndani na nje ya nchi," alisema Debora.

Ofisa wa TBS, Musa Luhombero, alisema lengo la elimu hiyo ni kusaidia bidhaa zinazozalishwa na wajasiriamali ambazo tayari zimethibitishwa kwa nembo ya ubora kuaminiwa na wateja.

Stella Mdemu, mjasirimali soko la sido alisema walishindwa kusajili nembo ya bidhaa zao wakihofia gharama za usajili na taarifa ya kwamba huduma hiyo inatolewa bure imeleta matumaini na watasajili.

Alisema elimu hiyo itakuwa na manufaa kwa wajasiriamali wengi kwani kabla walikuwa wakihofia gharama za kwenda kusajili bidhaa zao

## Zaidi wanafunzi 200,000 hupata elimu afya ya uzazi

Na Grace Mwakalinga

WANAFUNZI 203,000 wa shule za msingi na sekondari nchini kila mwaka hupata elimu ya afya ya uzazi, ushiriki wa masuala ya kiraia na mbinu mbalimbali za kujikwamua kiuchumi kupitia Shirika la Femina Hip. Kwa mujibu wa Naibu Mkurugenzi wa Shirika la Femina Hip, Amabilis Batamula, elimu hiyo huipata kwenye Jarida la Fema ambalo hutolewa na shirika hilo kwa ajili ya kuwasaidia wanafunzi kujifunza stadi mbalimbali za maisha.

Alisema awali jarida la Fema lilikuwa linatoka mara nne kwa mwaka na sasa ni mara tatu na hutolewa katika kila mkoa ukiwa na ajenda ambayo ina lengo ni kuelimisha jamii.

"Tunafurahi kuona ni sehemu ya mabadiliko ya vijana wetu, Jarida la Fema limekuwa nyenzo ya kufundishia mashule walimu hutumia kuwapatia maarifa mbalimbali watoto wetu hadi sasa tumewafikia vijana milioni saba," alisema Amabilis.

Alisema kwa sasa wanafunzi wana elimu ya kujitegemea ambayo imewawezesha kuanzisha shughuli zao za ujasiriamali baada ya kupata ujuzi kwenye Klabu za Fema shuleni.

Alisema wanafunzi wana uelewa wa kutosha kuhusu afya ya uzazi ambayo imewasaidia kukabiliana na vishawishi mbalimbali ambavyo vinaweza kuharibu ndoto za maisha yao kupitia elimu.

Mlezi wa Klabu ya Fema kutoka Sekondari ya Luiche, wilayani Kigoma, Elias Mulokozi alisema Jarida la Fema limewasaidia kushughulikia changamoto za wanafunzi wao.

Alisema jarida hilo limesheheni mambo mbalimbali yanawaongoza katika kushughulikia changamoto za vijana na aliwasihi walimu wengine kulitumia kama nyenzo ya kufundishia.

Kwa upande wake mlezi wa Klabu ya Fema, Nixon Lukaya kutoka Shule ya Sekondari ya Kigoma Grand, wilayani Kasulu Mkoa wa Kigoma alisema, vijana wake wameanzisha miradi mbalimbali ya kujiingizia kipato. Alisema wanafunzi waliojiunga na Klabu ya Fema wanafanya shughuli za kilimo cha migomba, mahindi na utunzaji wa misitu ambayo inatumika kwa ajili ya ufugaji wa nyuki.





# DSFA yakusanya bil.7.5/- miaka miwili ya Samia

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MAMLAKA ya Usimamizi wa Uvuvi wa Bahari Kuu (DSFA) imekusanya Sh. bilioni 7.5 kutokana na uuzaji wa leseni na shughuli za uvuvi zinazofanywa na meli za nje kwa kipindi cha mwaka 2021 hadi 2023.

Aidha, kwa mwaka wa fedha 2022/2023 mamlaka hiyo ilitarajia kukusanya zaidi ya shilingi bilioni tano, kwamba hadi sasa imeshakusanya Sh. bilioni nne na matarajio hadi kufikia Mei mwaka huu mamlaka hiyo inatarajia kukusanya Sh.bilioni tano.

Mkurugenzi Mkuu Mamlaka hiyo, Emmanuel Andrew Sweke, aliyasema hayo jana wakati akizungumza na wandishi wa habari kuhusu mafanikio ya sekta ya uvuvi wa bahari kuu ndani ya kipindi cha miaka miwili ya Rais Samia Suluhu Hassan.

Sweke alisema kiwango hicho ni kikubwa kulinganisha na kipindi cha mwaka 2017 hadi 2020 ambapo mamlaka ilishindwa kukusanya fedha kutokana na kutokuwepo kwa kanuni inayosimamia ununuzi wa leseni kwa upande wa mamkala hiyo Zanzibar sambamba na kujitokeza kwa ugonjwa wa corona.

"Fedha za leseni zilipunguza kutokana na kuwepo kwa mabadiliko ya kanuni ya uvuvi, sisi ni taasisi ya udhibiti wa shughuli za uvuvi katika bahari lakini baada ya kupatikana kwa kanuni mamlaka yetu inaruhusu uuzaji wa leseni", alisema.

Alisema kiwango hicho cha makusanyo ni kikubwa kulingaisha na kipindi cha mwaka 2017 hadi 2020 kutokana na kujitokeza kwa ugonjwa wa corona pamoja na kutokuwepo kwa kanuni ya uvuvi wa bahari kuu kwa upande wa Zanzibar.

Aidha, alisema kuwepo kwa programu yenye kutambua maeneo yenye samaki ambayo zaidi itawasaidia wavuvi wadogo kwa maeneo ya Wete, Pemba Unguja Tanga na maeneo mengine na zaidi ya wavuvi 400 watanufaika ambao tayari wamepatiwa mafunzo.

Katibu Mkuu Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi, Dk. Aboud Suleiman Jumbe, alisema mafanikio makubwa yaliyopatikana ndani ya kipindi hicho ni kutumika vyema kwa fedha za ugonjwa wa corona.

Alisema Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi ilitumia fedha hizo kwa ununuzi wa boti za kisasa za uvuvi pamoja na vifaa vya uvuvi walivyopatiwa wakulima na uvuvi wa samaki katika maeneo mbalimbali.

Jumbe alisema kuondolewa kero ya masuala ya uvuvi wa bahari kuu katika muungano ni mafanikio yaliyopatikana kwa kipindi cha miaka miwili ya Dk. Samia.

## Spika aridhishwa mchango wa NBC katika ustawi uchumi

**Na Mwandishi Wetu**

SPIKA wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Zubeir Ali Maulid amesema ameridhishwa na mchango wa Benki ya Taifa ya Biashara (NBC) katika ustawi wa uchumi visiwani Zanzibar.

Spika Zubeir alisema ameridhishwa na namna benki hiyo inavyoshirikiana na baraza hilo pamoja na serikali katika kuleta maendeleo visiwani Zanzibar kupitia huduma zake mbalimbali.

"Pamoja na yote hayo zaidi niwapongeze NBC kwa kuonesha umuhimu wa wateja wake kwa kurejesha miongoni mwa faida wanazozipata kwa namna mbalimbali ikiwemo kwa njia hii ya kufuturisha, uimarishaji wa huduma za afya, kuchangia afya ya uzazi salama pamoja na huduma nyingine kwa jamii tunashukuru," alisema.

Mkurugenzi wa Mikopo wa NBC, Salehe Mohamed alieleza kuwa hatua hiyo ni muendelezo wa utaratibu wa benki hiyo kwa miaka tisa ikilenga kujumuika na wateja wake kama hatua ya kuonyesha mshikamano na umoja katika kipindi cha Mwezi Mtukufu wa Ramadhani.

Alisema benki hiyo inaheshimu Mwezi Mtukufu wa Ramadhani kutokana na ukweli kwamba ni kipindi ambacho mwanadamu anajiweka karibu na Mungu kupitia mfungo na kufanya maombi.

Alisema kuwa benki hiyo ina huduma maalum inayojikita katika kutoa huduma kwa wateja wake wa imani ya Kiislam, yaani Islamic Banking inayopatikana kwenye matawi yote ikiendeshwa katika misingi ya dini.

Aidha aliwaomba wale ambao hawajajiunga na benki hiyo kufungua akaunti zao ili waweze kufurahia huduma bora na za kipekee zinazotolewa katika matawi yote ya NBC.




Spika wa Baraza la Wawakilishi, Zubeir Ali Maulid (wa pili kushoto) akiwaongoza wageni waalikwa pamoja na viongozi waandamizi wa Benki ya NBC kuomba dua ya chakula kwenye hafla ya futari iliyoandaliwa na benki hiyo kwa ajili ya wateja wake visiwani Zanzibar mwishoni mwa wiki. **PICHA: RAHMA SULEIMAN.**

## Wateja 30,000 wajiunga na CRDB Al Barakah

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya CRDB imesema kuwa wateja zaidi ya 30,000 wamejiunga na huduma za benki hiyo zinazofuata misingi ya sheria za "CRDB Al Barakah" katika kipindi cha mwaka mmoja tangu kuzinduliwa kwa huduma hizo.

Taarifa hiyo imetolewa juzi na Ofisa Mkuu wa Uendeshaji wa Benki ya CRDB, Bruce Mwile wakati wa hafla ya futari iliyoandaliwa na benki hiyo Zanzibar na kuhudhuriwa na wateja Zaidi ya 500.

Akitoa salamu maalum za Mwezi Mtukufu wa Ramadhan, Mwile aliwashukuru wateja kwa imani ambayo wameionyesha katika huduma za Benki ya CRDB zinazopatikana kupitia huduma hiyo.

"Idadi hii ya wateja ni ndani ya mwaka mmoja kuanzia 2021 tulipozindua kwa mara ya kwanza hadi tunafunga mwaka 2022. Haya ni mafanikio makubwa sana kwetu, lakini tunajivunia pia kufanya uwezeshaji wa zaidi ya Shilingi bilioni 73 kwa watu binafsi na biashara," alisema.

Aidha, aliwataka ambao hawajajiunga na mfumo huo wajiunge kwa sababu una huduma zinazogusa makundi yote ikijumuisha akaunti binafsi na za biashara.

Mwile alibainisha kuwa huduma za CRDB Al Barakah zinapatikana kupitia mtandao wa matawi ya benki hiyo kote nchini.

Akizungumza kwa niaba ya wateja wa benki hiyo, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji Zanzibar, Mudrick Soraga alipongeza Benki ya CRDB kwa mafanikio ambayo imeyapata kupitia mfumo wa CRDB Al Barakah.

Waziri Soraga alibainisha kuwa mfumo huo umesaidia kuchochea ujumuishi wa kifedha visiwani humo.

Hivyo, aliwataka Watanzania ambao wamekuwa nje ya mfumo rasmi wa kibenki kutokana na kukosa huduma zinazoendana na imani yao kuchangamkia fursa ya CRDB Al Barakah kujijenga kiuchumi.

Akielezea juu ya umuhimu wa kujitoa kipindi cha Mwezi Mtukufu wa Ramadhani, Waziri Soraga aliipongeza Menejimenti ya Benki ya CRDB kwa kuendeleza utamaduni wa kuuandaa na kushiriki futari na wateja, wadau na wenye uhitaji.

Aidha, aliwaasa wananchi kujikita katika ibada kwa kuishi kwa matendo mema katika kipindi hiki na baada ya Mwezi Mtukufu wa Ramadhan kwani matendo mema hayana ukomo wala kipindi maalum.

# PIC yaridhishwa utekelezaji miradi ya umeme vijijini

**Veronica Simba na Issa**

**Sabuni**

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (PIC), imesema imeridhishwa na utekelezaji wa miradi ya umeme vijijini mkoani Singida na kuwashauri wananchi waliofikiwa na huduma hiyo, kuitumia nishati hiyo kwa matumizi yenye tija hususani katika shughuli za kujiongezea kipato na kukuza uchumi.

Akizungumza na wananchi wa kijiji cha Irisya wilayani Ikungi, Mkoa wa Singida, wakati wa ziara ya Kamati hiyo kukagua maendeleo ya utekelezaji wa Mradi wa Kusambaza Umeme Vijijini Awamu ya Tatu Mzunguko wa Pili (R3R2), Aprili Mosi 2023, Makamu Mwenyekiti wa PIC, Augustino Vuma, alisema lengo la serikali kupeleka umeme vijijini ni kuwarahisishia wananchi kutekeleza kwa ufanisi shughuli mbalimbali za kiuchumi ili wajiletee maendeleo badala ya kurudisha nyuma juhudi hizo za serikali.

Aliwaagiza Watendaji wa Wakala wa Nishati Vijijini (REA) kuendelea kuwasimamia kwa ukaribu makandarasi wanaotekeleza miradi ya umeme vijijini ili kuhakikisha wanafanya kazi kwa kuheshimu mikataba yao na kufanikisha azma ya serikali kuwafikishia umeme wananchi wote waishio vijijini waweze kujikwamua kiuchumi.

Katika hatua nyingine, Makamu Mwenyekiti wa PIC ameeleza kuwa Kamati imeridhishwa na utekelezaji wa Mradi wa R3R2 huku akibainisha kuwa tayari manufaa yake yameanza kuonekana.

"Leo tumekuwa hapa katika Shule ya Sekondari Irisya na tumeshuhudia kwa macho yetu wanafunzi wameshaanza kunufaika kwani umeme umeingia kwenye maabara na kufika katika madarasa hivyo kuwawezesha kujisomea hata nyakati za usiku."

Alisema Kamati imeshuhudia umeme katika maabara ya Fizikia na nyinginezo na kuwawezesha wanafunzi kusoma kwa vitendo.

Vilevile, kuhusu manufaa kwa wananchi, umeme umeanza kuwafikia kuwawezesha kufanya shughuli za kiuchumi ikiwamo kuanzisha viwanda vidogo.

Mwenyekiti wa Bodi ya Nishati Vijijini (REB), Janet Mbene pamoja na kuunga mkono uhamasishaji wananchi kuunganisha umeme katika makazi na shughuli za kiuchumi, amesema ni faraja kwa REA kuona umeme unaendelea kuwafikia wananchi katika maeneo mbalimbali vijijini.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti mbele ya Kamati ya PIC, Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba na Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Irisya, Ernest Edward, wametoa shukrani kwa serikali kupitia REA kwa kufikisha umeme katika kijiji hicho.

Awali, akiwasilisha taarifa ya utekelezaji wa miradi ya umeme vijijini mkoani Singida kwa Kamati, Mkurugenzi Mkuu wa REA, Mhandisi Hassan Saidy, alisema serikali kupitia wakala hiyo imetoa Sh. bilioni 73.1 na Dola za Marekani 988,707.60 kuhakikisha miradi minne inayotekelezwa mkoani humo inakamilika na wananchi wanapatiwa huduma ya nishati hiyo ili kujipatia maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

Alisema Mradi wa Umeme Vijijini awamu ya tatu mzunguko wa pili katika wilaya za Ikungi na Singida unatekelezwa na Mkandarasi M/s Central Electricals International Ltd kwa gharama ya Sh. bilioni 26.3 na katika Wilaya za Iramba, Manyoni na Mkalama, unatekelezwa na M/s CRJE - CTCE Consortium kwa gharama ya Sh. bilioni 31.6.

Alisema, maendeleo ya mradi kwa wastani yamefikia asilimia 70.21 na kwa wilaya za Ikungi na Singida, Mkandarasi amefikia asilimia 77.54 na Wilaya za Iramba, Manyoni na Mkalama, Mkandarasi amefikia asilimia 62.87.

Mkoa wa Singida una jumla ya vijiji 441 na vijiji 287 vimepatiwa umeme kupitia miradi ya REA iliyotekelezwa awali. Vijiji 169 vilivyobaki vinaendelea kuunganishiwa kupitia wakandarasi waliotajwa.



Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (PIC), wakikagua utendaji kazi wa maabara ya Fizikia katika Shule ya Sekondari Irisya, wilayani Ikungi, Mkoa wa Singida, baada ya kuunganishiwa umeme kupitia Mradi wa Usambazaji Umeme Vijijini awamu ya tatu mzunguko wa pili. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Wapewa tahadhari majanga yanayoleta mabadiliko tabianchi

**Na Hamisi Nasri,** MASASI

WAKAZI wa Wilaya ya Masasi, mkoani Mtwara wamehimizwa kuchukua tahadhari dhidi ya majanga yanayosababishwa na athari za mabadiliko ya tabianchi ikiwamo uharibifu wa mazingira.

Wito huo ulitolewa jana na Mratibu wa maafa wa halmashauri ya mji, Bibie Abdukarim alipofanya mikutano ya wazi na wananchi wa kata za Mkomaindo kupitia mtaa, Rest Camp, Mkuti na kata ya Napupa, stendi kuu ya mabasi Masasi na stendi ndogo ya TK iliyopo barabara kuu ya kuelekea Wilaya ya Newala.

Alisema madhara ya uharibifu wa mazingira ikiwamo kukata miti ovyo, utupaji taka za plastiki na kusababisha baadhi ya madhara kwa mifugo pia zinapochomwa moto vibaya moshi wake husababisha magonjwa ya mapafu.

Alisema kuna kila sababu ya kutunza mazingira ili kuepuka athari za uharibifu wa mazingira zinazosababishwa na mabadiliko ya tabianchi hivyo ni lazima jamii iwe na uelewa wa kutosha na mwamko chanya wa kupanda miti kwa wingi kwenye maeneo yao wanayoishi ikiwa ni hatua ya kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Abdukarim alisema kuna faida kubwa za kutunza mazingira ikiwa ni upatikanaji wa mvua za kutosha, majisafi na salama, hewa safi, ardhi yenye rutuba ambayo hupelekea mavuno ya kutosha.

Alisema ukataji miti kupisha shughuli za maendeleo ya kijamii na kiuchumi kama ujenzi wa barabara, nyumba, shule, viwanda na shughuli za kilimo na inashauriwa jamii inapokata miti pia inapaswa kupanda kwa wingi ili kuepuka athari.

Alisema zipo njia kadhaa za kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi ikiwamo uharibifu wa mazingira na moja wapo ni pamoja na kupanda miti na kuacha kuharibu vyanzo vya maji na kulima mazao yanayostahimili ukame.

# TAKUKURU yaanzisha programu kupambana na rushwa

**Na Steven William, MUHEZA**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Wilaya ya Muheza imeanza kuwashirikisha wananchi katika programu mpya ya TAKUKURU rafiki pamoja na kutoa elimu ya mapambano dhidi ya rushwa.

Mkuu wa TAKUKURU wilayani hapo, Joseph Mkumbi, aliyasema hayo juzi katika taarifa yake kwenye mkutano wa utambuzi na uchambuzi wa kero za wananchi katika Kata ya Kwafungo na maeneo mengine.

Alisema eneo la mikutano hiyo ni kutoa elimu kwa wananchi kutambua athari za rushwa na kuwashirikisha katika programu hiyo.

Alisema kuwa programu hiyo imeandaliwa na TAKUKURU kwa lengo la kuimarisha na kuongeza ushiriki wa jamii na wadau katika mapambano dhidi ya rushwa.

Alisema kuwa mikutano hiyo ina lengo la utekelezaji wa programu hiyo kupitia kata zote na vijiji wilayani Muheza, mwaka huu na kuanzia Kata ya Kwafungo.

Diwani wa Kata ya Kwafungo, Gabriel Mswagala, alisema programu hiyo mpya itasaidia sana kutoa taarifa za vitendo vya rushwa.

Wananchi walimpongeza mkuu wa TAKUKURU wilaya ya Muheza kwa kuwapa elimu ya athari za rushwa na kuleta programu hiyo mpya ili kuwafichua watu wanaopenda kuomba rushwa na wanaotoa.

HABARI KIMATAIFA

# Serikali yaitahadharisha Azimio maandamano Kenya

**NAIROBI,** Kenya

NAIBU Rais Nchini Kenya Rigathi Gachagua ametoa onyo kali kwa waandamanaji wa muungano wa Azimio akisema kuwa leo hali itakuwa tofauti endapo ghasia zitajirudia, akisisitiza kwamba serikali itatoa makucha yake.

Akizungumza mwishoni mwa wiki katika eneo la Magharibi, Rigathi alisema kinachoshuhudiwa wakati wa maandamano hayo ni uhalifu ambao hautakubaliwa na serikali.

Katika maandamano yaliyoitishwa na kiongozi mkuu wa upinzani nchini Kenya, Raila Odinga, ikiwa ni wiki ya tatu sasa kumekuwa kukishuhudiwa uhalifu wa wizi, uharibifu wa mali na kufungwa kwa shughuli za kiuchumi.

**Sheria za nchi hii zinajulikana vizuri. Haya si maandamano ila ni ghasia za baada ya uchaguzi, uporaji na wizi wa kimabavu.**

"Jumatatu 'leo' itakuwa siku ya mwisho kwa wale ambao watahusika katika uporaji wa mali, nataka niwaonye vijana ambao wanatumia maandamano na ghasia zinazopangwa na Odinga kuiba mali na kupora watu. Jumatatu 'leo' itakuwa ni siku ya mwisho kufanya hivyo," alisema Rigathi.

Aliongeza kuwa serikali itakuwa imara kuhakikisha kuwa wafanyabiashara na mali zao zinakuwa salama, huku akimrai Odinga kuwa anachoendesha sasa ni ghasia za baada ya uchaguzi, na kwamba serikali itatoa makucha yake.

"Sheria za nchi hii zinajulikana vizuri. Haya si maandamano ila ni ghasia za baada ya uchaguzi, uporaji na wizi wa kimabavu," alisema Rigathi.

Aidha, aliashiria kuwa polisi watakabiliana na waandamanaji wa Azimio vikali leo endapo wataendeleza ghasia hizo.

"Haya ni makosa ambayo adhabu yake inajulikana vizuri. Serikali sasa itatoa makucha yake ili kulinda maisha na mali ya watu kupitia kutekeleza sheria vilivyo," alisema. **KTN**

## Majeshi Somaliland yakabiliana na wanamgambo

**LAS'ANOD,** Somalia

MAPIGANO mapya baina ya majeshi ya Somalia na wanamgambo wa kieneo yamezuka katika mji unaogombaniwa wa Las'anod nchini Somalia, ikiwa ni miezi miwili baada ya serikali ya Marekani kutaka kuondolewa kwa wanajeshi katika eneo hilo.

Kwa mujibu wa VOA Majeshi ya Somaliland yalipambana na wanamgambo wa kieneo katika mji wa Las'anod mwishoni mwa juma lililopita. Inaelezwa kuwa kwa kiasi cha siku 50, pande hizo mbili zimejihusisha katika mapigano ambayo yameuwa zaidi ya watu 200 na kuwajeruhi zaidi ya 600.

Wananchi katika eneo hilo la Las'anod wamezitaka mamlaka ikiwemo serikali kuu ya Mogadishu kusitisha mzozo huo, huku Somaliland ikisisitiza kuwa eneo hilo liko chini ya udhibiti wake.

Aidha, serikali ya Marekani ilishauri kwamba Somaliland ni vyema iondoe majeshi yake kutoka Las'anod ili kufungua njia kwa majadiliano na suluhisho kwa mzozo huo.

Hata hivyo, mamlaka Somaliland ilisema kuwa serikali ya Marekani haijaishinikiza serikali ya Puntland kuacha kupeleka wapiganaji kwenda huko Las'anod.

Vile vile, vyombo vya habari vya ndani na watumiaji wa mitandao ya kijamii, walibandika picha Jumamosi ambazo zilimuonyesha mbunge wa zamani wa Puntland Farah Mohamed Dalmar akiwa chini ya ulinzi wa Somaliland baada ya kukamatwa. **VOA**



Wakimbizi wa Somalia waliokimbia mapigano huko Lasscanood, Somaliland, wakiwa katika kambi ya muda huko Qoriley katika mkoa wa Somali Ethiopia. **PICHA: VOA**

# Kitendawili makubaliano ya demokrasia Sudan

**KHARTOUM,** Sudan

MSEMAJI wa mchakato wa kisiasa unaowaleta pamoja wanajeshi na raia nchini Sudani, Khaled Youssef, amesema zoezi la utiaji saini wa makubaliano kati ya raia na wanajeshi limeahirishwa hadi Aprili sita, mwaka huu.

Katika taarifa yake aliyoitoa mwishoni mwa juma lililopita, Youssef alisema makubaliano hayo yanastahili kuzindua upya mpito wa kidemokrasia nchini Sudan na kufanya uwezekano wa kurejea katika hali ya awali kabla ya mapinduzi ya kijeshi ya Oktoba 2021.

Utiaji saini huo ulipangwa awali kufanyika Jumamosi lakini kuahirishwa kwake kulitangazwa na Youssef, mmoja wa maofisa wa kiraia waliofukuzwa kazi na kukamatwa wakati wa mapinduzi ya Jenerali Abdel Fattah al-Burhane.

"Mzozo juu ya mambo ya kiufundi yanayohusiana na mageuzi ya vikosi vya usalama uliwalazimisha wahusika wakuu kukubaliana siku tano za ziada za mazungumzo, hadi Aprili 6, mwaka huu," alisema Youssef.

Aliongeza kuwa hati ya mwisho ya makubaliano inalenga kuweka wazi mambo muhimu ya mpito kwa serikali ya kiraia na hatimaye uchaguzi wa taasisi za kidemokrasia.

Alisema kwa wiki kadhaa, wanajeshi, wanamgambo na raia wamekuwa wakijadili maswala tata, hasa yale ya haki ya mpito na mageuzi ya vikosi vya usalama.

Aidha, inaelezwa kwamba suala lenye matatizo zaidi linaonekana kuwa jinsi ya kujumuisha Vikosi vya Msaada wa Haraka (RSF), ambavyo vingi vinaundwa na wanamgambo wa zamani, katika vikosi vya serikali.

Hata hivyo, inabainishwa kuwa kinyume na hali ya mzozo wa madaraka, hali hiyo pia inagawanya viongozi wa juu akiwemo Jenerali Burhane na wa pili wake mkuu Mohamed Daglo, ambaye ni mkuu wa RSF.

Vile vile, vikosi vya RSF ambavyo vinaundwa na wanamgambo wa Janjawid, wanaotuhumiwa kwa ukatili wakati wa vita vya muda mrefu na vibaya vilivyoanza mwaka 2003 huko Darfur (magharibi), vinashutumiwa pia kuhusika katika ukandamizaji wa uasi dhidi ya dikteta Omar Al-Bashir, ulioanzishwa mwishoni mwa 2018 na kumalizika Aprili 2019. **RFI**

## IMF kuipatia Ukraine dola bil-15

**KYIV,** Ukraine

SHIRIKA la Fedha la Kimataifa (IMF) limeidhinisha mpango wa msaada wa dola bilioni 15 kwa Ukraine, mpango uliotiwa saini wiki mbili zilizopita na serikali ya Kyiv.

Ilielezwa kuwa mpango huo ni sehemu ya bahasha kubwa ya dola bilioni 115. Na kwamba kuthibitishwa kwa msaada huo mpya kunaruhusu kutolewa kwa awamu ya kwanza ya dola bilioni 2.7.

Ilibainishwa kuwa lengo la usaidizi huo mpya wa dola milioni 15.6 mwanzoni, ni kuwezesha Ukraine kuunganisha bajeti yake ya mwaka 2023, lakini pia kuimarisha rasilimali zake za kifedha na kupunguza mfumuko wa bei.

Kwa mujibu wa IMF, msaada huo wa jumla ya bilioni 115 kwa kipindi cha miaka minne, unavipengele vitatu ikiwemo bilioni 2 katika kufutwa kwa sehemu ya deni lililopo, msamaha wa madeni wa bilioni 20, mikopo ya bilioni 60 na misaada ya bilioni 20.

Aidha, ilieleza kuwa kwa msaada huo, Ukraine inapaswa kuhakikisha kuanza maisha mapya baada ya vita na ujenzi mpya.

"IMF inatarajia kufufua uchumi taratibu mwaka huu nchini Ukraine. Lakini pia inaona hali mbaya zaidi, ikiwa vita vitaendelea hadi mwisho wa mwaka 2025." ilisema.

Ukraine imeungwa mkono na taasisi za kifedha tangu kuanza kwa mashambulizi ya Russia Februari 24, 2022. Benki ya Dunia ililipa dola bilioni 20, Marekani dola bilioni 110, ikiwa ni kwa msaada wa kijeshi.

Hiyo imeruhusu nchi kuweka huduma zake za umma sawa ikiwemo kulipa mishahara ya watumishi wa umma. **RFI**

HABARI MICHEZO

# SHIKANGWA AMRITHI OPA KWA MABAO LIGI KUU WANAWAKE

**Na Adam Fungamwango**

STRAIKA wa Simba Queens, Jentrix Shikangwa, amemrithi mwenzake aliyekuwa akicheza naye kwenye timu hiyo, Opa Clement kwa kuongoza kwa ufungaji kwenye Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania Bara, akifikisha mabao 10 hadi sasa

Opa, ambaye ameuzwa na klabu yake ya Simba Queens hivi karibuni kwenda nchini Uturuki kuichezwa Besikitas alikuwa ndiye kinara wa mabao hadi anaondoka akiwa amecheka na nyvu mara tisa.

Aliyekuwa pacha mwenzake kwenye timu hiyo, Shikangwa raia wa Kenya, amefikisha mabao 10, akiwa amechukua nafasi yake ya ufungaji kwenye kikosi cha Simba Queens na Ligi Kuu pia.

**Wakati Shikangwa akiwa na mabao 10, wachezaji watatu akiwamo Opa ambaye pia ni straika wa Timu ya Taifa ya Tanzania, Twiga Stars, wana mabao tisa kila mmoja.**

Wachezaji hao ni Donisia Minja wa JKT Queens na Cynthia Musungu raia wa Kenya ambaye naye ametimkia Uturuki katika timu hiyo ya Opa, akiwa ameacha mabao yake tisa kwenye Ligi Kuu.

Winfrida Charles wa Alliance Girls ana mabao manane, huku wachezaji saba wakiwa na mabao matano kila mmoja.

Wachezaji hao ni Stumai Abdallah, Fatuma Mustapha na Jacline Shija wote wa JKT Queens, Blessing Nkor wa Yanga Princess, Jamila Rajab wa Baobab na Priviledge Mupeti wa Fountain Gate Princess.

Wakati huo huo, timu ya Mbagala Queens imeendelea kufanya kweli kwenye Ligi ya Soka Wanawake Mkoani Dar es Salaam ikifikisha jumla ya pointi 12, ikishinda mechi zote nne ilizocheza.

Msimamo wa ligi hiyo unaonyesha kuwa timu ya Mabibo Queens inashika nafasi ya pili kwa kuwa na pointi tisa, The Eleven Star Queens ya tatu kwa pointi hizo hizo tisa, Sayari Women ikiwa kwenye nafasi ya nne kwa pointi hizo.

Timu hizo tatu zinapishana mabao ya kufunga, huku pia Youngstars Queens ikiwa kwenye nafasi ya tano kwa pointi saba na Evergreen Queens ya sita na pointi saba pia.

Kinondoni Queens inakamata nafasi ya nane ikiwa na pointi nne, Wisdom Queens nafasi nne pia, Ubungo Tafseo Queens ya tisa kwa pointi nne pia, Ubungo Tafseo Queens ya 10 kwa pointi zake tatu.

Tanzanite Princess iko kwenye nafasi ya 11 bila kuwa na pointi, Ukonga Queens ikiburuza mkia nayo ikiwa haina pointi yoyote.

## MAMILIONI YA MAMA...



Meneja Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally (wa pili kulia), akikabidhi Sh. milioni tano kwa Nahodha wa klabu hiyo, John Bocco, baada ya kuzipokea kutoka kwa Msemaji Mkuu wa Serikali, Gerson Msigwa (kulia) kwa niaba ya Rais Samia Suluhu Hassan, ikiwa ni ahadi yake ya kutoa kiasi hicho cha fedha kwa kila goli litakalofungwa na Simba na Yanga kwenye michuano ya kimataifa, Ligi ya Mabingwa na Kombe la Shirikisho Afrika. Simba juzi ilikubali kipigo cha mabao 3-1 ugenini dhidi ya Raja Casablanca ya Morocco, na iliporejea katika Uwanja wa Julius Nyerere, Dar es Salaam jana, Msigwa aliwakabidhi kitita hicho. **PICHA: SAADA AKIDA**

# Musonda: Yanga imenipeleka timu ya taifa

**Na Adam Fungamwango**

STRAIKA Mzambia Kennedy Musonda, amesema Klabu ya Yanga imemsaidia kuitwa kwenye timu ya taifa kwa mara ya kwanza akiwa kama mchezaji anayesakata soka la kulipwa nje ya nchi, hivyo anajivunia kuwa kwenye kikosi hicho.

Musonda ambaye amesajiliwa kipindi cha dirisha dogo msimu huu akitokea Klabu ya Power Dynamos ya kwao Zambia, alisema alishawahi kuitwa huko nyuma kwenye timu ya taifa, lakini alikuwa ni mchezaji wa timu zinazocheza ndani ya nchi, ila safari hii anacheza soka la kulipwa nje ya nchi.

"Najivunia kuwa kwenye klabu hii kwa sababu imenisaidia kuitwa kwenye timu yangu ya taifa kwa mara ya kwanza nikiwa mchezaji ninayecheza soka la kulipwa nje ya nchi, huko nyuma nilishawahi kuitwa, lakini nilikuwa mchezaji wa ndani, kwa sasa tupo kwenye hali nzuri na kikosi chetu na tunataka kufuzu Fainali za Mataifa ya Afrika (Afcon) kwa sababu tumeshindwa kufanya hivyo kwa miaka ya karibuni.

"Nafikiri Yanga imenisaidia kwa sababu ya hii michuano ya Kombe la Shirikisho barani Afrika hatua ya makundi, ni michuano mikubwa watu wengi wanaifuatilia, makocha Yanga wakanipa nafasi na mchango wangu umeonekana, hivyo hakukuwa na njia nyingine kwa wakubwa wa soka Zambia na benchi la ufundi zaidi ya kunijumuisha kwenye kikosi," alisema.

Alisema malengo waliyojiwekea msimu huu ni kutwaa ubingwa wa Tanzania Bara, na kuendelea kufanya vema kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho kiasi cha kuifanya Yanga kuwa moja ya timu tishio barani Afrika.

Awali, straika huyo hakukubalika kwa wapenzi na mashabiki kutokana na kuonekana kutozoea mazingira na pia mfumo, lakini ghafla ameotokea kuwa tishio na kuanza kuwa kipenzi cha baadhi ya mashabiki wa Yanga.

# Azam FC, Mtibwa ni ushindi tu FA leo

**Na Saada Akida**

MICHUANO ya Kombe la Shirikisho la Azam (ASFC) maarufu FA Cup, itaanza kutimua vumbi rasmi leokwa Azam FC kuikaribisha Mtibwa Sugar katika Uwanja wa Azam Complex uliopo Chamazi, Dar es Salaam.

Azam FC baada ya kushindwa kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara imesema nguvu zao wamezielekeza katika mchezo wa leo wa hatua ya robo fainali dhidi ya Mtibwa Sugar.

Lakini pia Mtibwa Sugar nao wamedhamiria kufanya kweli katika mchezo huo, wakitafuta ushindi mbele ya wapinzani wao hao ili kusonga mbele hatua inayofuata ya nusu fainali.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Msaidizi wa Azam FC, Kali Ongala, alisema wanatambua umuhimu wa mashindano hayo na wako tayari kwa ajili ya kuwakabili Mtibwa Sugar.

Alisema wanafahamu mchezo huo utakuwa wa ushindani mkubwa kwa sababu kila mmoja wao anahitaji kuvuka hatua hiyo na kusonga mbele kucheza robo fainali.

"Wachezaji wetu wako tayari kwa ajili ya mchezo wa kesho (leo) dhidi ya Mtibwa Sugar, itakuwa mechi ngumu, tutacheza kwa tahadhari kubwa ili kufikia malengo yetu ya kuvuna ushindi," alisema Ongala.

Naye Kocha Mkuu wa Mtibwa Sugar, Salum Mayanga, alisema wamejiandaa vizuri, hawana majeruhi na wachezaji wake wako tayari kusaka ushindi katika mchezo huo wa leo.

Aliongeza kuwa ni mechi ngumu kwa sababu wanacheza na timu nzuri na bora, lakini anaamini mpira ni dakika 90 na atakayefanya makosa ataadhibiwa.

"Safari hii tumedhamiria kufanya kweli kwenye Kombe la Shirikisho, tunatambua mechi itakuwa ni ngumu kwa sababu tunahitaji kusonga mbele katika michuano hii ili kuweza kuwa sehemu ya timu nne zitakazoshiriki michuaono ya kimataifa," alisema Mayanga.

**Safari hii tumedhamiria kufanya kweli kwenye Kombe la Shirikisho, tunatambua mechi itakuwa ni ngumu kwa sababu tunahitaji kusonga mbele.**

## ZISIKUPITE

### MESSI NA MSIMAMO PSG

MSHAMBULIAJI wa Argentina, Lionel Messi, mwenye umri wa miaka 35, hatapunguza mshahara wake ili kubaki Paris St-Germain. ***(Goal)***

### GVARDIOLA KWA CITY, MADRID

MANCHESTER City na Real Madrid wamemfanya mlinzi wa RB Leipzig mwenye umri wa miaka 21 raia wa Croatia, Josko Gvardiol, kuwa mlengwa wao huku thamani yake ikitajwa kuwa ni pauni milioni 75. ***(90min)***

### MOUNT ANYATIWA LIVER

LIVERPOOL na Manchester City, zote zinawania kumsajili kiungo wa kati wa England, Mason Mount, mwenye umri wa miaka 24, kutoka Chelsea msimu huu wa majira ya joto, huku 'Wekundu' hao kwa sasa wakionekana kuwa mstari wa mbele. ***(Football Insider)***

### POCHETTINO HATAKIWI SPURS

MWENYEKITI wa Tottenham Hotspur, Daniel Levy, amemwambia kocha wa zamani wa timu hiyo, Mauricio Pochettino, hataki Muargentina huyo kurejea katika klabu hiyo. ***(Star)***

### CHELSEA KULIPA MAMILIONI

CHELSEA inakabiliwa na uwezekano wa kuwalipa wachezaji mamilioni ya fedha ili kuondoka katika klabu hiyo msimu huu wa majira ya joto huku wakipania kupunguza dau lao la mishahara. ***(Sun)***

### UNITED YAMFUATILIA FELIX

KLABU ya Manchester United inafuatilia hali ya mshambuliaji wa Atletico Madrid na Ureno, Joao Felix, mwenye umri wa miaka 23, ambaye kwa sasa yuko kwa mkopo Chelsea. ***(Mundo Deportivo)***

### FATI AWANIWA MAN CITY

KLABU ya Manchester City inalenga kumsajili Ansu Fati wa Barcelona mwenye umri wa miaka 20, baada ya maoni yaliyotolewa na baba wa fowadi huyo wa Hispania kuhusu kukosa muda wa kucheza. ***(Football Insider)***

### ANCELOTTI ATAKIWA BRAZIL

KOCHA Carlo Ancelotti raia wa Italia amethibitisha kuwa Brazil wanataka kumteua kama kocha wao, hata hivyo anataka kusalia Real Madrid. ***(ESPN)***

### SANCET AOTA MBAWA

MATUMAINI ya Aston Villa kumsajili kiungo wa kati wa Hispania, Oihan Sancet kutoka Athletic Bilbao yamepata pigo baada ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22, kusaini mkataba mpya wa muda mrefu na klabu hiyo ya LaLiga. ***(TeamTalk)***


### LAPORTE ATAKIWA SPURS

KLABU za Tottenham Hotspur na PSG zimepewa fursa ya kumsajili beki wa Hispania, Aymeric Laporte, 28, kutoka Manchester City. ***(90 Minutes )***

### MAN YATAKA MAKIPA

MANCHESTER United inamtaka golikipa wa Porto, Diogo Costa, 23 na David Raya mwenye miaka 27 wa Brentford. ***(Express)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# ARTETA AKUNWA NA MBIO ZA ARSENAL EPL

**LONDON,** England

MIKEL Arteta alisifu umakini wa Arsenal huku viongozi hao wa Ligi Kuu England wakirejesha faida yao ya pointi nane kwa ushindi dhidi ya Leeds United kwenye Uwanja wa Emirates, Jumamosi.

**Uongozi wa Arsenal kwenye kilele ulipunguzwa hadi pointi tano baada ya ushindi wa Manchester City wa 4-1 dhidi ya Liverpool mapema Jumamosi, lakini kikosi cha Arteta kilirejesha matokeo hayo dhidi ya Leeds.**

Gabriel Jesus alifunga mara mbili huku Ben White na Granit Xhaka pia wakifunga, ambapo hawakuwa na Bukayo Saka tangu mwanzo kwa mara ya kwanza kwenye Ligi Kuu msimu huu.

> ●●● Tulifahamu matokeo ya Man City kama ni mchezo mkubwa, na tulitaka kutazama...

Arteta, ambaye alifichua kuwa fowadi huyo wa England aliwekwa benchi kutokana na kuugua Ijumaa, alifurahishwa na jinsi wachezaji wake walivyobaki wakizingatia kazi waliyonayo.

"Tulikuwa na mambo machache yanayoendelea na baadhi ya watu binafsi. Imekuwa siku chache kuhusu sababu hatukuweza kuamua hadi asubuhi kama baadhi ya wachezaji wangepatikana na kupangwa," aliiambia BBC.

"Baada ya mapumziko ya kimataifa, hujui kama wako katika akili ya kurejea na kufanya mambo muhimu ili kushinda ligi hii. Hakika nimefurahishwa na mwenendo.

"Tulifahamu matokeo ya Man City kama ni mchezo mkubwa, na tulitaka kutazama sehemu zake. Lakini tulipofika hapa, ilikuwa ni kutuangazia tu na nini tunaweza kufanya kama timu. Tunaweza tu kudhibiti kile tunachoweza kufanya."

Bosi huyo wa 'Washikabunduki' pia alimsifu Jesus, ambaye alifunga mabao mawili katika mechi yake ya kwanza tangu arejee kutoka kwenye majeraha.

"Nina furaha sana kwake baada ya kazi yote kutoka kwake," Arteta alisema.

"Leo (juzi) alipata zawadi kwa hilo. Analeta ubora na kutotabirika kwenye kikosi."

LIVE IN PLAY
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 536,

MECHI KALI
EVERTON
VERSUS
TOTTENHAM
1 | 3.19
X | 3.19
2 | 2.16

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# CHELSEA MAMBO SI MAMBO

**LONDON,** England

MABAO kutoka kwa mshambuliaji Ollie Watkins na nahodha John McGinn, yaliipatia Aston Villa pointi zote tatu katika ushindi wa 2-0 dhidi ya Chelsea, Jumamosi na kuifanya timu hiyo kuendelea kuwa kwenye wakati mgumu.

Matokeo hayo yaliipeleka Villa katika nafasi ya tisa kwenye msimamo, na kuwaruka Chelsea hadi nafasi ya 11 (kabla ya mechi za jana Jumapili).

Watkins alifunga dakika ya 18 baada ya makosa ya beki Marc Cucurella, ambaye alipiga kwa kichwa mpira kuurudisha nyuma na kisha kuuwahi na akapiga shuti lake kwa utulivu na kumfunga kipa Kepa Arrizabalaga.

Chelsea, walimiliki mpira kwa asilimia 69, lakini mara nyingi walikosa meno mbele ya lango. Kelele za mashabiki zilisikika pale Stamford Bridge wakati timu ikiwa nyumbani na Graham Potter aliyeonekana kuhuzunika akiondoka uwanjani, shinikizo likiwa limerejea kwenye mabega yake.

Timu yake itaikaribisha Liverpool Jumanne na itacheza na Real Madrid katika robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya baadaye mwezi huu.

"Lazima tukubali matokeo na kufanya vizuri zaidi," Potter aliiambia Sky.

"Hatuwezi kujihurumia. Tuna mchezo mzuri Jumanne wa kujiweka sawa," aliongeza Potter.



# Carlo Ancelotti athibitisha kutakiwa kuinoa Brazil

**MADRID,** Hispania

CARLO Ancelotti amethibitisha kuwa Timu ya Taifa ya Brazil inataka kumteua kama kocha, lakini amesisitiza nia yake ya kubakia Real Madrid.

Brazil imekuwa bila kocha mkuu tangu Tite alipoondoka baada ya Kombe la Dunia 2022 na ripoti mbalimbali zinadai Ancelotti ndiye lengo lao kuu.

Mshambuliaji wa Madrid, Vinicius Jr wiki iliyopita alisema "anaamini" kocha wa klabu yake anataka kuchukua kazi kwa 'Selecao' hao na Ancelotti anafurahishwa na nia hiyo.

"Ukweli ni kwamba timu ya taifa ya Brazil inanitaka; naipenda hiyo, inasisimua," Ancelotti aliwaambia wanahabari kabla ya mchezo wa Madrid dhidi ya Real Valladolid.

"Kutoka hapo, lazima uheshimu mkataba ulionao, ambao nataka kuutimiza."

Ancelotti mwenye umri wa miaka 63, ana mkataba na Madrid hadi mwaka 2024. Alirejea katika klabu hiyo kwa kipindi cha pili cha kuinoa 2022 na kuwaongoza 'Los Blancos' kutwaa LaLiga na Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu uliopita.

Mwaka huu, Madrid wako pointi 12 nyuma ya vinara Barcelona kwenye LaLiga, lakini wamesalia kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya na Kombe la Mfalme.

Mustakabali wake unatarajiwa kuhusishwa na jinsi Madrid wanavyofanya katika mashindano hayo mawili, ingawa amesisitiza kwamba anataka kubaki Santiago Bernabeu.

## HABARI MICHEZO


,262,050

JACKPOT
MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 05/04/23 | 21:15 | Perugia vs Reggina | 2.52 | 2.94 | 2.83 |
| 02. 05/04/23 | 21:45 | RB Leipzig vs Borussia Dortmund | 2.29 | 3.60 | 2.90 |
| 03. 05/04/23 | 22:00 | Barcelona vs Real Madrid | 2.29 | 3.21 | 2.96 |
| 04. 05/04/23 | 22:00 | West Ham vs Newcastle | 3.00 | 3.25 | 2.22 |
| 05. 06/04/23 | 01:00 | Danubio FC vs SC Emelec | 2.38 | 3.05 | 2.84 |
| 06. 06/04/23 | 02:00 | Huachipato vs Union Espanola | 2.40 | 3.21 | 2.69 |
| 07. 06/04/23 | 03:05 | Pumas De Tabasco vs Zacatepec | 2.89 | 3.36 | 2.19 |
| 08. 06/04/23 | 05:00 | Deportivo Pereira vs Colo Colo | 2.58 | 3.08 | 2.58 |
| 09. 06/04/23 | 19:00 | Slask Wroclaw vs GKS Piast Gliwice | 2.43 | 3.09 | 2.67 |
| 10. 06/04/23 | 22:15 | El Ittihad Alexandria vs Coca Cola | 2.86 | 2.91 | 2.56 |
| 11.07/04/23 | 03:00 | FBC Melgar vs Olimpia Asuncion | 2.25 | 3.13 | 2.98 |
| 12. 07/04/23 | 03:00 | CA Tigre vs Sao Paulo | 2.54 | 3.06 | 2.64 |
| 13. 07/04/23 | 08:00 | Western United vs Central Coast Mariners | 2.68 | 3.26 | 2.47 |

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMATATU - 03/04/2023

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:30 | 4872 | Lampang vs Bangkok Glass | 4.83 | 3.86 | 1.55 |
| 15:00 | 4635 | Ethiopian Medhin vs Arba Minch Kenema | 2.29 | 2.90 | 3.15 |
| 16:30 | 4650 | Pusamania Borneo vs Bali Utd Pusam | 1.94 | 3.49 | 3.24 |
| 17:30 | 2618 | NK Jarun Zagreb vs Rudes Zagreb | 3.43 | 3.12 | 2.01 |
| 18:00 | 2555 | Dire Dawa Kenema FC vs Legetafo Legedadi | 1.62 | 3.52 | 5.07 |
| 19:00 | 1074 | AEK Larnaca vs Apoel Nicosia | 2.44 | 3.15 | 2.84 |
| 19:00 | 2056 | EN Paralimni vs Doxa Katokopia | 2.20 | 3.23 | 3.17 |
| 19:00 | 2116 | Maccabi Petach Tikva vs Hapoel Acre | 1.59 | 3.80 | 5.28 |
| 19:00 | 2384 | Paide Linnameeskond vs FCI Levadia Tallinn U21 | 5.31 | 4.78 | 1.49 |
| 19:00 | 3679 | FC Versailles 78 vs Chateauroux | 2.20 | 3.15 | 3.20 |
| 19:00 | 5936 | Resovia Rzeszow vs GKS Tychy | 2.27 | 3.17 | 2.82 |
| 19:30 | 3223 | Concarneau vs Sedan | 1.79 | 3.41 | 4.31 |
| 19:30 | 3394 | Empoli vs Lecce | 2.43 | 3.00 | 2.90 |
| 20:00 | 1098 | Hapoel Rishon Lezion vs SC Kfar Qasem | 2.47 | 3.10 | 2.84 |
| 20:00 | 1331 | Jonkopings Sodra vs Orebro SK | 2.48 | 3.26 | 2.78 |
| 20:00 | 1446 | El Fahem vs Bnei Yehuda | 2.11 | 3.22 | 3.38 |
| 20:00 | 2189 | Aarhus vs Randers | 1.95 | 3.34 | 3.79 |
| 20:00 | 2666 | B36 Torshavn vs HB Torshavn | 2.82 | 3.23 | 2.24 |
| 20:00 | 2681 | Hapoel Afula vs Hapoel Ramat Gan | 2.09 | 3.27 | 3.38 |
| 20:00 | 2806 | Penafiel vs Porto B | 2.27 | 3.22 | 2.91 |
| 20:00 | 2819 | Orgryte IS vs AFC Eskilstuna | 1.95 | 3.61 | 3.56 |
| 20:00 | 3349 | Stal Mielec vs Jagiellonia | 2.36 | 3.14 | 2.73 |
| 20:00 | 3695 | Ingolstadt vs 1860 Munich | 2.52 | 3.48 | 2.52 |
| 20:00 | 5147 | Mjallby vs Varbergs Bois | 1.89 | 3.24 | 3.65 |
| 20:10 | 2054 | Elfsborg vs BK Hacken | 2.78 | 3.40 | 2.19 |
| 20:15 | 1283 | Beitar Jerusalem vs Hapoel Haifa | 2.15 | 3.24 | 2.98 |
| 20:30 | 1737 | Eyupspor vs Erzurum BB | 1.56 | 3.64 | 5.13 |
| 20:30 | 1777 | Oostende U21 vs St Truiden U21 | 2.12 | 3.00 | 3.00 |
| 20:30 | 2784 | Sepsi Osk vs Steaua Bucuresti | 2.78 | 3.15 | 2.42 |
| 20:30 | 4312 | Istanbulspor vs Fatih Karagumruk | 3.01 | 3.48 | 2.15 |
| 20:30 | 5634 | Altay vs Sakaryaspor | 2.67 | 3.24 | 2.34 |
| 21:00 | 1086 | Jong PSV vs Roda Kerkrade | 2.71 | 3.39 | 2.32 |
| 21:00 | 2679 | Jong Ajax vs Dordrecht | 1.57 | 4.18 | 4.60 |
| 21:00 | 3961 | Almere City vs Jong Utrecht | 1.38 | 4.67 | 6.43 |
| 21:00 | 5478 | Jong AZ Alkmaar vs De Graafschap | 3.12 | 3.54 | 2.03 |
| 21:00 | 5867 | MTK Budapest vs Nyiregyhaza | 1.42 | 4.54 | 5.36 |
| 21:30 | 2146 | Renate vs Calcio Lecco | 2.43 | 3.09 | 2.98 |
| 21:30 | 2727 | Brown Adrogue vs Atletico Rafaela | 2.36 | 2.91 | 3.01 |
| 21:45 | 1309 | Guingamp vs Bordeaux | 3.11 | 3.16 | 2.22 |
| 21:45 | 1755 | Sassuolo vs Torino | 2.36 | 3.10 | 2.90 |
| 21:45 | 5328 | York City vs Barnet | 2.43 | 3.42 | 2.63 |
| 22:00 | 2895 | Everton vs Tottenham | 3.19 | 3.19 | 2.16 |
| 22:00 | 3289 | Albacete Balompie vs Las Palmas UD | 2.51 | 2.97 | 2.82 |
| 22:00 | 4639 | Valencia vs Rayo Vallecano | 2.08 | 3.05 | 3.55 |
| 22:00 | 5108 | Racing Club (URU) vs Defensor Sporting | 3.45 | 3.19 | 1.98 |
| 22:15 | 1740 | Haras EL Hodood vs Enppi Club | 2.55 | 2.90 | 2.85 |
| 22:15 | 3667 | Famalicao vs FC Arouca | 1.96 | 3.27 | 3.72 |
| 22:15 | 5582 | Ismaily SC vs Ceramica Cleopatra | 3.07 | 2.87 | 2.44 |
| 23:00 | 3316 | AD Grecia vs Santos Guapiles | 2.09 | 3.21 | 3.21 |
| 23:10 | 4808 | CA Atlanta vs Mitre SdE | 2.15 | 2.92 | 3.42 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


# RAGE AIPA MBINU SIMBA KUTINGA NUSU FAINALI CAF

Na Adam Fungamwango

RAIS wa zamani wa Klabu ya Simba, Ismail Aden Rage, amefanya kikao na benchi la ufundi la timu hiyo pamoja na wachezaji na kuwapa mbinu ambayo itawasaidia kwenye mechi inayofuata ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

**Rage ambaye alikuwa nchini Morocco kushuhudia mechi ya kukamilisha hatua ya makundi kati ya timu hiyo na Raja Casablanca, Simba ikifungwa mabao 3-1, amesema kitakachowasaidia kwenye mechi zinazofuata si kukaba njia tena bali ni kwa staili ya mtu kwa mtu 'police marking', ambayo anaona itawabeba zaidi kwenye mechi zinazofuata.**

"Mpira ulipokwisha nilikwenda kutoa ushauri wangu, nikaongea na walimu na baadhi ya wachezaji na nimewaambia wajitahidi kwenye michezo inayokuja kufanya aina ya ulinzi inayoitwa mtu kwa mtu, 'police marking', badala ya kukaba njia, yaani wakati mnashambuliwa mnahakikisha wale wapinzani wenu hawawi peke yao, hamkai nao mbali, ili wasijiandae na kufanya wanachokitaka wakati wanapokuwa na mpira, mkiwa nao mbali, inakuwa ni hatari, lakini mkiwa nao karibu kidogo tu mpira mnawadhibiti, nina imani kabisa kuwa watafanya jitihada hizo," alisema Rage.

Kwenye mechi hiyo iliyochezwa usiku mnene wa Aprili Mosi, Rage alisema Simba ilicheza vema lakini kulikuwa na matatizo upande wa ulinzi ndiyo yaliyofanya wapoteze.

"Simba wamecheza vizuri, lakini wamepoteza mchezo, kwenye soka hili lipo, unaweza kucheza vizuri, lakini ukafungwa, matatizo makubwa yalikuwa ni kwenye upande wa ulinzi, ambapo walifanya makosa hayo hayo na timu hii tulipocheza Dar es Salaam na ndiyo maana nikawapa hiyo mbinu, lakini mimi binafsi nilishtuka sana nilivyoona kiwango kile cha Simba, kilikuwa kizuri sana nikielewa hali halisi ya wachezaji wetu tuliokuwa nao, tunakwenda robo fainali, lakini kikubwa zaidi ni kwamba katika mashindano mengine makubwa yanayokuja tunatakiwa tujiimarishe kwenye sehemu ya ulinzi, viungo wakabaji na safu ya ushambuliaji iongezwe nguvu," alishauri.

Kikosi cha Simba kilirejea nchini jana na kinasubiri keshokutwa, Jumatano droo ya michuano hiyo itakapopangwa na Shirikisho la Mpira wa Miguu Afrika (CAF), ili kujua itacheza na timu gani kwenye hatua ya robo fainali ambapo itaanzia nyumbani Uwanja wa Benjamin Mkapa na kwenda kumalizia ugenini.

Baada matokeo ya makundi yote kukamilika juzi, Simba itacheza na timu kati ya Wydad Casablanca ya Morocco ambao ni vinara wa Kundi A, Mamelodi Suudowns ya Afrika ya Kusini ikiliongoza Kundi B au Esperance ya Tunisia, ambao wapo kileleni kwenye Kundi D.

## Robertinho hesabu

INATOKA UK. 24

Katika hatua nyingi Msemaji wa Serikali, Gerson Msigwa, akikabidhi zawadi ya Sh. milioni tano ikiwa ni ahadi ya Rais Samia Suluhu Hassan ya kutoa kiasi hicho kwa kila goli litakalofungwa na Simba na Yanga kwenye michuano ya kimataifa msimu huu, alisema amekabidhi fedha fedha hizo ikiwa utekelezaji ya Mama.

"Nimekuja kukabidhi hizi fedha nina imani itakuwa chachu kwa wachezaji kuendelea kufanya vizuri katika hatua inayofuata ya robo fainali," alisema Msigwa.

Meneja wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alimshukuru Rais Samia na kumuahidi kupambana kuhakikisha wanampeleka Mama nusu fainali.

Aliongeza kuwa baada ya droo ya Jumatano watamfahamu mpinzani wao na Aprili 21 au 22, mwaka huu, wataanza kutupa karata yao katika hatua ya robo fainali.

"Tunamkaribisha Mama Aprili 21 au 22, kuja kuwashuhudia watoto wake wakipambana, lakini kuja kuwakabidhi fedha kwa mikono yake katika mchezo wetu wa kwanza wa robo fainali tutakaocheza Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam," alisema na kuongeza:

"Safari yetu ilikuwa sehemu kubwa na mambo mengi, lakini tunamshukuru Mungu tumefika na tumecheza mechi bora sana hasa jinsi ya wachezaji walicheza vizuri.

"Licha ya kupoteza mechi tumeridhika, hivyo tumejifunza na tunajua jinsi gani ya kucheza, sasa tunasubiri droo ipangwe, maana tunayemtamani na sisi anatutamani," alisema Ahmed.



Aden Rage

## *Yanga yaweka rekodi*

INATOKA UKURASA 24

ambaye alionekana mwiba upande wa Yanga mpaka pale alipoumia katikati ya kipindi cha pili, alipowalamba chenga wachezaji wanne wa Yanga kabla ya kuachia shuti kali lililopanguliwa na kipa Mnata na kuwa kona.

Straika tegemeo wa Yanga, Fiston Mayele hakuwa kwenye mchezo mzuri jana na alionekana dakika mbili kabla ya mechi kumalizika, alipowazidi mbio mabeki wa TP Mazembe, lakini kabla ya kuingia ndani ya eneo la hatari alichezewa madhambi.

Metacha alifanya tena kazi ya ziada dakika za majeruhi, alipopangua mpira uliokuwa ukielekea wavuni kwa kichwa kilichopigwa na Cristian Kouame na hadi mwisho matokeo yalibaki kuwa TP Mazembe 0-1 Yanga.

# Michezo

Jumatatu Aprili 3, 2023

Nipashe




Chelsea mambo si mambo UKURASA 22

TUMEMALIZA...



Fiston Mayele (kushoto) na Kennedy Musonda, wakimpongeza Farid Musa (katikati), baada ya kuifungia Yanga bao pekee wakati ikishinda 1-0 dhidi ya TP Mazembe kwenye mechi ya kukamilisha hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho Afrika iliyopigwa katika Uwanja wa TP Mazembe uliopo Lubumbashi, DR Congo jana. Yanga ilishuka uwanjani hapo ikiwa tayari ifuzu hatua ya robo fainali kutoka Kundi D sambamba na US Monastir ya Tunisia, ambayo jana usiku ilikuwa ikicheza dhidi ya Real Bamako ya Mali. **MPIGAPICHA WETU**

## Robertinho hesabu daraja Yanga CAF

**Na Saada Akida**

BAADA ya kikosi cha Simba kurejea nchini kikiwa na uhakika wa kucheza robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Kocha Mkuu wa Simba, Robertinho Oliveira, amesema sasa nguvu zao wanazielekeza katika michezo mitatu ya Kombe la Shirikisho la Azam na Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Yanga.

Simba imerejea nchini jana kutokea Morocco kwenye mchezo wao wa kukamilisha hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Raja Casablaca ambao ilikubali kipigo cha mabao 3-1, lakini hata hivyo, timu hizo zote zilishafuzu robo fainali katika Kundi lao la C.

Akizungumza na Nipashe baada ya kutua nchini, Robertinho, alisema mechi hizo mbili ni sehemu ya maandalizi ya kuelekea mchezo wao wa robo fainali ya Ligi ya Mabingwa ambapo mpinzani wao watamjua keshokutwa, Jumatano.

Robertinho alisema mechi mitatu za nyumbani ikiwamo michezo miwili dhidi ya Ihefu FC mchezo wa Kombe la FA na mechi ya Ligi dhidi ya Yanga ataitumia kwa ajili ya kujiandaa na michezo yao miwili ya robo fainali.

Alisema wachezaji wake hawakucheza vibaya kwenye mechi iliyopita dhidi ya Raja Casablanca na kwamba walicheza vizuri na kuonesha  kiwango kizuri, licha ya kufungwa.

"Nimefurahi kuona Simba imefuzu kucheza hatua ya robo fainali licha ya kupoteza mchezo dhidi ya Raja Casablanca, sasa akili na nguvu tunazielekeza kwenye mechi zilizopo mbele yetu ikiwa ni pamoja na kushinda dhidi ya Yanga na kucheza nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa.

"Kuhusu wachezaji wangu wawili Mohammed Hussein (Tshabalala) na Sadio Kanoute ambao hawakuwapo mechi iliyopita, sasa nitaungana nao kuelekea mechi zetu zijazo kuhakikisha tunafikia malengo," alisema Robertinho.

INAENDELEA UKURASA 23

# Yanga yaweka rekodi Afrika

**Na Adam Fungamwango**

●●● Yakaa kileleni ikisikilizia matokeo ya Watunisia baada ya kuvunja mwiko TP Mazembe kwa...

BAO la dakika ya 63 lililowekwa wavuni na mtokea benchini, Farid Mussa, jana liliiwezesha Yanga kuweka rekodi ya kuwa timu ya kwanza Tanzania kuifunga TP Mazembe ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, kwenye uwanja wake wa nyumbani, jijini Lubumbashi.

**Simba ilitua jijini humo kucheza dhidi ya TP Mazembe kwenye hatua ya raundi ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa ikafungwa mabao 3-2 mwaka 2011, halafu ikaenda tena msimu wa 2018/19 kwenye mechi za makundi ligi hiyo ikatandikwa mabao 4-1.**

Yanga nayo mwaka 2016 ilikwenda Lubumbashi na kuchapika kwa mabao 3-1, mechi ya Kombe la Shirikisho barani Afrika hatua ya makundi.

Awali, Februari 19, mwaka huu, Yanga ilikuwa timu ya kwanza nchini kuifunga TP Mazembe, ilipopata ushindi wa mabao 3-1 kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa katika mfululizo wa mechi za Kombe la Shirikisho barani Afrika Kundi D.

Mpira wa krosi iliyopigwa na Jesus Moloko, ulionekana kama utadakwa kirahisi na kipa Narcisse Nlend, lakini pamoja na kuuchupia, ulimponyoka na kuangukia miguuni mwa mfungaji Farid, ambaye hakuwa na kazi kubwa sana zaidi ya kuupiga na kujaa wavuni.

Farid alikuwa ameingia kuchukua nafasi ya Mudathir Yahaya aliyetolewa baada ya kupata kadi ya njano mapema kipindi cha kwanza cha mchezo huo na kutolewa kipindi cha pili.

Kwa matokeo hayo, pamoja na kwamba Yanga tayari ilishafuzu, lakini imefikisha jumla ya pointi 13 na kuendelea kuliongoza kundi hilo ikisubiri matokeo ya mechi ya US Monastir itakayokuwa nyumbani Tunisia dhidi ya Real Bamako ndiyo yataamua timu gani kati ya hizo itakayoongoza kundi lao.

Yanga itaendelea kuwa kileleni kama US Monastir itapoteza, sare au kufunga mabao yasiyozidi mawili, lakini kama itashinda 3-0 na kuendelea Watusia hao wataongoza kundi hilo.

Kwenye mechi hiyo wenyeji walianza kulisalimu lango la wegeni wao dakika ya nne tu pale Ismail Ganiyu alipopiga kichwa mpira wa krosi ya Glory Likonza, ukatoka nje.

Yanga ilijibu shambulizi hilo dakika mbili baadaye, Moloko alipofanikiwa kuingia ndani ya eneo la hatari na kupiga krosi ambayo ilimkuta Kennedy Musonda, akamtengea Mudathir aliyekuwa anakuja kwa kasi, kabla ya kupiga shuti ambalo liliishia kwenye mikono ya golikipa Nlend.

Kipa Metacha Mnata alilazimika kufanya kazi ya ziada dakika ya 12 alipochupa na kuukamata mpira ulliopigwa na Joel Beya ambaye alimegewa pande na Ernest Luzolo.

Almanusra TP Mazembe iandike bao dakika ya 24 baada ya Isama Mpeko kuruka juu na kuunganisha mpira wa faulo iliyopigwa na Luzolo, mpira ukampita kipa Metacha, lakini badala ya kujaa wavuni ukatoka sentimeta chache.

Kipindi cha pili, pamoja na timu zote kufanya mabadiliko, zilishambuliana kwa zamu, lakini safu zao za ushambuliaji zilikuwa butu.

Ilikuwa ni dakika mbili tu baada ya mapumziko, Luzolo

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002